ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
49.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nne – Tarehe 15 Oktoba, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani mswada wa sheria ya kuanzishwa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Abdalla Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Katiba na Utawala): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria wa kuanzishwa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJI BU

Nam. 33

Ujenzi wa Soko la Kuuzia Samaki Mpakanjia

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Jimbo la Mtambwe ni jimbo ambalo wananchi wake wametawanyika katika vijiji mbali mbali kando kando ya bahari; na hivyo ni wavuvi wakubwa sana, lakini hadi hii leo bado hawana soko la kuuzia samaki kama ilivyokuwa miaka mingi iliyopita. Kwa sababu Wizara yako kwa kupitia mfuko wa TASAF huwa inatoa msaada wa fedha kujenga masoko sehemu kadhaa.

Je, Wizara haioni kuwa iko haja ya wananchi hawa na wao kusaidiwa kwa kutumia mfuko huu kujengewa soko katika kijiji cha Mpakanjia/Uondwe ili na wao waweze kutumia soko hilo kwa manufaa yao badala ya kuuza samaki wao chini ardhini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhni yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam 33 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kutumia fursa hii kuwapongeza sana wavuvi wa Jimbo la Mtambwe kwa umahiri wao na juhudi kubwa wanazozichukua ambazo huchangia sana katika kukuza pato la Taifa na kupunguza umasikini wa kipato.

Mhe. Spika, ninapenda kukubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kuwa ipo haja ya wavuvi na wananchi wa eneo hili kuwa na soko maalum la kuuzia samaki wao.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa ninamuomba Mhe. Mwakilishi kuwahamasisha wananchi ili waweze kuibua mradi wa soko kupitia mradi wa TASAF au kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ni dhahiri suala hili linahitaji mashirikiano yetu sote ili kuweza kupata ufumbuzi muafaka kwa manufaa ya wananchi na wavuvi wa Jimbo la Mtambwe. Hivyo mara tutakapopata maombi hayo yatashughulikiwa ipasavyo ili kuondoa tatizo hilo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, ninashukuru sana kupata jibu la matumainio lakini Mhe. Spika, ninavyoelewa, ni kuwa tunayo Kamati ya Maendeleo ya Jimbo la Mtambwe ambayo iliwahi kupeleka ombi lake kwenye Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais iliyoko Pemba kwa sababu ya kusaidiwa ujenzi wa soko hilo, na wao wako tayari kutumia nguvu zao ili kuona kuwa suala hili limefanikiwa. Lakini kwa bahati mbaya mpaka leo hatujapata jibu lolote na ndio sababu ya kuuliza swali hili.

Kwa hivyo kwa vile aliyoyaelekeza Mhe. Waziri tumeshayafanya sijui ananambia vipi zaidi kuwa tukumbushe halafu tushirikiane ili soko tuweze kulijenga, kwa sababu inaumiza kuona mahala watu leo wanauza samaki wakiondoka mbwa wanakuja wanakunya na kadhalika, siku ya pili panauzwa pale pale ni hatari wala si ubinaadamu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu mama kwamba wananchi wanatakiwa kuibua mradi huo na kuyawasilisha maombi hayo kupitia ima TASAF au Wizara inayohusika na Maendeleo ya Uvuvi na Mifugo. Na kwa kuwa Mhe. Salim amesema tayari amelipeleka suala hili katika Ofisi yetu iliyopo Pemba, nitahakikisha ninalifuatilia jambo hilo ili kuona ombi lenyewe, ikiwa ombi lenyewe linakidhi haja, taratibu zitafuata ili tuhakikishe kwamba ujenzi huo unafanyika katika eneo hilo kwa nia ile ile ya kuwasaidia wananchi wetu ili wapate soko la kisasa na kufanya shughuli zao za kuuzia samaki.

Nam. 36

Malipo ya Dharura kwa Madaktari na Manesi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Madaktari na Manesi wetu wamekuwa wakifanya kazi ngumu kwa kujitolea na hata kuhatarisha maisha yao na baadhi ya wakati hufanya kazi nje ya muda wao wa kazi kutokana na uhalisia wa shughuli zao.

(a) Madaktari na manesi hao hulipwa kiasi gani pale wanapoitwa kuja kufanya kazi wakati wa dharura nje ya muda wao wa kazi.

(b) Ni sababu gani zinazopelekea manesi na madaktari hao kutolipwa malipo yao kutokana na kufanya kazi huko wakati wa dharura.

(c) Wizara haioni kutowalipa kwa wakati ndio kunawarudisha nyuma au kuwavunja moyo madaktari na manesi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako Tukufu suali lake lenye vifungu a, b, na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Kwanza ningependa kutoa shukurani zangu kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza ningependa kutoa shukurani zangu kwa wafanyakazi wa Wizara ya Afya na wasaidizi wao, madereva, watu wa *ambulance* wanafunzi wa afya, *red cross* na vikosi vya ulinzi kwa jinsi wanavyokuwa tayari wakati inapotokea dharura, na Serikali inafarijika sana kwa hili.

Vile vile naomba niwashukuru watu binafsi pamoja na mashirika na taasisi mbali mbali yanavyokuwa tayari kusaidiana na Serikali yetu wakati wa dharura inapotokea.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo sasa najibu suali.

a) Wakati wa dharura inapotokea, wito hutolewa na Wizara ya Afya kwa wafanyakazi wote wanaokua kazini na hata wanaokuwa likizo na wastaafu pia huitwa ili kukabiliana na dharura iliyotokea, na hapa ndipo suala la wito linapokuja kwa wafanyakazi wa afya. Wafanyakazi wa Afya hatupaswi kudai malipo kwa sababu hilo ni kinyume na maadili yetu.

b) Kwenye Bajeti ya Wizara ya Afya kifungu kwa ajili ya kulipa wafanyakazi wakati wa dharura hatuna wala hatuombi, kwa sababu kitengo cha maafa kiko chini ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Wizara hua inaomba fedha za dharura Serikalini pale tu inapotokea dharura kwa ajili ya kununua vifaa na dawa ili tujipange kutoa huduma.

c) Mshahara na maposho ndio haki ya mfanyakazi. Kwa vile dharura ni hali inayojitokeza bila ya taarifa, kinachozungumzwa hapa ni shukurani ya Serikali yetu kwetu baada ya kuona kwamba tumefanya kazi nzito iwape chochote wafanyakazi hao kama inazo fedha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri yalokidhi swali la msingi, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Hivi karibuni tumeshuhudia matokeo mawili muhimu na tukawaona wauguzi wetu na madaktari wetu. Kuna taarifa tu kuna mfuko wa maafa ulikuwa umetolewa kwa waokoaji kwa siku elfu ishirini na tukawatizama madaktari wetu na manesi wetu wameacha nyumba zao na wao walikuwa na umuhimu. Je, walifidiwa kiasi gani Mhe. Naibu Waziri?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri katika swali lake la msingi kwamba masuala yanayohusiana na mambo ya maafa yanasimamiwa na Idara Maalum kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Spika, serikali kwa sasa haijakuwa na mfuko maalum unaoshughulikia mambo ya maafa isipokuwa pale panapotokea maafa hatua za dharura huchukuliwa kwa Wizara inayosimamia mambo ya maafa ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuwaandikia Wizara ya Fedha kuomba fedha maalum kwa ajili ya shughuli hiyo.

Kwa upande wa madaktari hakuna fedha zilizotolewa kwa ajili ya kuwasaidia madaktari kwenye suala hili la dharura. Isipokuwa fedha zilizosaidia ni zile ambazo ma-*diver* binafsi waliojitolea kusaidia shughuli zile za uokoaji ndio hawa ambao walipewa fedha ya shilingi elfu ishirini kwa siku. Kwa madaktari watalipwa kutokana na taratibu zao za kazi, na kama kuna suala la *overtime* litalipwa kutokana na muda wao wa o*vertime.* Lakini hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya dharura kwa madaktari kwenye shughuli ya uokoaji hasa wanapohudumia waokoaji wale wanaotokea katika dharura ya maafa. Ule ni wajibu wao kama ni madaktari kusaidia wananchi wenzao na kufanya wajibu wao wa kikazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili napenda kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa swali la msingi limezungumzia mafao ya madaktari wetu pamoja na manesi hususan pale wanapofanya kazi za ziada, na kwa kuwa ni ukweli usiofichika Mhe. Spika, kwamba madaktari wetu na hawa wauguzi wanafanya kazi wakati mwengine katika mazingira ya hatari hususan katika kipindi hiki cha gonjwa la ukimwi je, Mhe. Naibu Waziri anaweza akatueleza kwamba kuna *risk allowance* yoyote wanayolipwa ma-*surgeon* wanapofanya *operation* na hawa manesi pale wanapozalisha hususan kwa vile hususan kwa vile wanatumia mikono na vifaa ambapo *possibility* na wao kuambukizwa magonjwa mabaya kama yapo je, mnawalipa risk *allowance* au mnawaachia tu. Na kama hamuwalipi lolote katika mazingira kama haya si ndio sababu madaktari wanatukimbia hapa nchini kukimbilia nchi za jirani ili kuweza kulipa mafao ya ziada.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza nataka niseme swali lako liko nje ya swali mama, lakini nitakujibu kwa faida yako. Suala la afya, wafanyakazi wa afya tunafundishwa kila jambo, maradhi hatarishi na yasiyokuwa hatarishi na jinsi gani ya kujikinga. Si ukimwi tu unaoambukiza kuna mengi ambayo huyafahamu yanaambukiza, lakini tunapofundishwa tunajua kwamba tutakabiliana na tatizo gani linapotokea tatizo kama hilo. Suala la Ukimwi hakuna hata mfanyakazi mmoja wa afya asiyejua jinsi gani ya kujikinga, wanafundishwa wananchi wa kawaida seuze wanaotoa huduma.

Sasa kusema kwamba tupewe *risk allowance* kwa ukimwi itabidi tupewe *risk allowance* kwa kifua kikuu, itabidi tupewe *risk allowance* kwa maradhi yote yanayoambukiza. Kwa hivyo *risk allowance* haiambatani na maradhi gani ambayo tunayoyatibu. *Risk allowance* ni posho ambayo inatakiwa itengenezwe kwa kujali maslahi ya wafanyakazi wetu. Lakini sio kwa sababu ya ukimwi.

Suala la *overtime* hilo linatakiwa kulipwa lakini wakati wa dharura hatupaswi kulipwa kama tunalipwa tulipwe kwa sababu kipo kwa kutuonea huruma kwamba hawa wafanyakazi wamejitahidi lakini hata wakitulipa utalala siku mbili, mimi nimeshawahi kulala siku mbili na siku tatu nikashinda ofisini. Ina maana nimekaa pale masaa 56 ukinipa shilingi elfu kumi italipa hailipi tuwasaidie wananchi wetu tusiichagize serikali pale ambapo hapana dharura.

Nam. 64

Ukosefu wa Taa katika Bustani ya Donge

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Katika Bustani ya Donge iliyopo eneo la Darajani kwa muda mrefu kumekuwepo na kero ya ukosefu wa taa nyakati za usiku na kusababisha baadhi ya watu kufanya vitendo visivyofaa ikiwemo vya mapenzi.

(a) Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ina mpango gani wa kuondoa tatizo hilo.

(b) Kwa kuwa vitendo vinavyofanyika huwa vinakwenda kinyume na mila na utamaduni wa Zanzibar, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha ulinzi katika bustani hiyo na ile ya Jamhuri ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, Naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam 64 (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba bustani iliopo pale Mkunazini njiapanda (maarufu bustani ya Donge) watu wengi hupenda kupumzika baada ya harakati zao za kazi za mchana kutwa, na lazima nikiri kwamba ni kweli kuna ukosefu wa taa nyakati za usiku na kusababisha kero kwa wananchi wetu.

(a) Mhe. Spika, baada ya kubaini tatizo hilo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza la Manispaa hivi sasa tayari linaendelea na kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya Mpango wa kuunga umeme na kuweka taa katika eneo hilo la bustani ya Donge. Baadae juhudi zitafanyika kutafuta fedha zitakazogharamia kazi hiyo ya uwekaji wa taa.

Tayari mpango kama huo tumeshaanza na tumeukamilisha pembezoni mwa bustani ya Jamhuri na Mhe. Jaku mwenyewe ninafikiri anaona kidogo taa pale pembezoni mwa barabara *opposite* na *Haile Selassie* taa zinawaka. Kwa hivyo tunarajia mpango kama ule nao tuufanye kwa bustani ya Donge.

(b) Mhe. Spika, Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi katika bustani zote mbili ile ya Donge na Bustani ya Jamhuri ili kuhakikisha vitendo visivyokubalika na ni kinyume na mila, silka na utamaduni wa Zanzibar vinadhibitiwa na yoyote atakayehusika na uhalifu huo tutamchukulia hatua kali za kisheria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mafupi sana ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza. Lini serikali itatekeleza ahadi yake kwa vitendo katika bustani ile ya Donge ambayo tumekuwa tukiipigia kelele kwa muda mrefu na wakati huu hasa hivi vitendo vimezidi.

Na pili wakati bustani ile iko katika eneo la Mji Mkongwe kuna bustani iko Gofu vile vile Mhe. Waziri wakati wa jioni pale panawekwa magari je, imekuwa ni *showing* ya magari kuuza pale.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, Mhe. Spika, siwezi kusema tarehe gani lakini hii ni changamoto tunaichukua kulikamilisha hili, hii kero ya bustani ya Donge ni kweli kwamba ni kero nakubaliana na yeye na kama nilivyosema tuko katika mchakato, kwa hivyo tutajitahidi kulitimiza hilo.

Kuhusu magari ni kweli pale mahala pamegeuzwa nasikia panaitwa kwa jina la jabalali pale, magari yanauzwa pale yanapakiwa yanauzwa. Sasa hiyo ni kinyume na utaratibu ndio yale ninayozungumza siku zote tunajitahidi Baraza

la Mji tuna kitengo chetu cha mipango miji tunajitahidi sana haya mambo kuyarekebisha lakini tunapambana na upinzani mkali. Sasa Mhe. Jaku kwa umaarufu wako na uzoefu wako nakuomba na wewe utusaidie kuwashawishi hao wanaoekeza pale magari ya kuuza watafute yadi nyengine. Ni mwahala mwingi mmewekwa yadi mnauzwa magari lakini pale si mahali pake.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninamuomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kuwa bustani zile za wananchi madhumuni yake makubwa ni kuwafanya watu wakae pale wapumzike wapate hewa safi, wanaokaa pale ni watu na heshima zao, lakini kwa kuwa bustani hizi sasa zote takriban zimekuwa zinatumika visivyo, kuna mapenzi ya ovyo yanayofanywa mule, na kwa kuwa kufanya hivi ni kukiuka sheria za nchi hii je Mhe. Waziri anaweza kunambia ni kesi ngapi zimepelekwa mahkamani na ni watu wangapi waliopatikana na hatia na kuhukumiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa kweli sina takwimu za hivyo vitendo alivyovieleza Mhe. Abdalla. Lakini ukweli kwamba hivyo vitendo vinafanyika. Kwa sababu walinzi wangu wale wa bustanini wamenihakikishia hasa kweli na wanaofanya hayo ni vijana wetu wanakwenda pale na mafaili yao wanasema wenyewe wanafanya *discussion* lakini *discussion* hiyo inafanywa kizani hakuna taa na unapowaendea tena wanatawanyika. Sasa kidogo hali haipendezi. Hili kama ni wazee na sisi tuchukue jukumu tuwanasihi watoto wetu, pale bustani imeruhusiwa wakapumzike wafanye *discussion* lakini kwa mchana. Na haya mengi yanatendeka usiku na hatua moja nimesema ni hiyo ya kuweka taa, lakini tutaimarisha ulinzi wetu tuone mambo kama haya kwa kweli yasifanyike kututia aibu katika hii niliyosema silka na utamaduni wetu.

Takwimu hatuna lakini tutaimarisha tuone kwamba mambo haya hayafanyiki.

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa amekiri vitendo visivyofaa vinafanyika katika maeneo hayo, na kwa kuwa hakuna hata mtu mmoja ambaye alotiwa hatiani. Lakini je alikuwa anasubiri ushahidi kamili na lini atueleze hapa siku atopata huo ushahidi kamili na kuchukuliwa hatua vijana hao wanaofanya vitendo visivyofaa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba hatujamtia mtu hatiani na wakati huo wote tulikuwa tunafanya mambo kidogo na sisi kuwaasa wale wanaofanya yale waache, lakini sasa imekuwa kwa kweli mambo kidogo yamefuturu ada hali inatisha. Sasa ninakuhakikishia Mhe. Mtumwa tutajitahidi sasa tuwakamate na tuwatie hatiani hao wahalifu. Lakini mengine hayahitaji ushahidi huo unaousema yako wazi kabisa.

Nam. 4

Kuanzishwa Mfumo wa Kuvuna Maji ya Mvua

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa maji ni rasilimali muhimu kwa maisha ya binadamu, na kwa kuwa bila maji hakuna maisha, na kwa kuwa Zanzibar tunapata mvua misimu miwili kwa mwaka na hatimae maji haya hupotea baharini.
Je, ni lini Serikali itaanzisha miundombinu ya kuvuna maji ya mvua na hatimae kuyaingiza kwenye mfumo wa maji safi kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake nambari 4 kama ifuatavyo:-

Naomba kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa maji ni rasilimali muhimu katika maisha ya mwanadamu, na bila ya maji hakuna maisha na kwa kulijua hilo Serikali kupitia Wizara yangu imeliona hilo na imechukua juhudi kwa kiasi kikubwa kwa kuanzisha miradi mbali miradi hiyo, na pamoja na mradi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira unaofadhiliwa na Serikali, AFDB na UN-HABITAT ambapo miongoni mwa vipengele vya mradi huo ni kipengele cha uvunaji wa maji ya mvua, hadi sasa tayari mafunzo juu ya uvunaji wa maji ya mvua yameshafanyika na

imetenga maeneo ya Skuli ya Muungano, Pete na Mgambo kwa Unguja na Kilindi na Kisiwani kwa Binti Abeid Pemba kwa ajili ya majaribio ya Mradi huo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwanza nishukuru tu kwamba serikali kupitia nchi wafadhili wameshaanza kutaka kufanya majaribio ya kuvuna maji ya mvua katika baadhi ya maeneo ya visiwa vyetu viwili vya Unguja na Pemba, lakini Mhe. Spika, kwa sababu wenzetu wa Bara hapo wanachimba malambo sisi tunaita mabwawa, wanachima malambo ambao hukusanya maji siku za mvua na hatimae yakasaidia kwa ajili ya mifugo. Na kwa kuwa wao hawatumii wafadhili, kwa sababu mradi wenyewe hauna fedha nyingi ni mawasiliano tu wanaweza kufanya mashimo yale ili tukaweza kupata hayo maji.

Je, ni lini serikali yetu hii ya *GNU* inayoongozwa na Rais wetu kipenzi Dr. Ali Mohammed Shein kupitia Wizara hii ya Mawasiliano ikachimba mabwawa katika vijiji kadhaa vya nchi hii ili kuhifadhi maji yale ambayo yanapotokea siku za mvua na hatimae yakatusaidia kwa kunyweshea ng'ombe wetu pamoja na kilimo cha mbogamboga ambacho ni sera yetu ya *GNU proverty reduction* na *income generative* kuweza kuifanya vilivyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ushauri wa Mheshimiwa ni mzuri naona bora niupokee kama ni ushauri isipokuwa ninamueleza tu kwamba kuna tofauti ya ardhi, ardhi ambayo ina mawe na ardhi ambayo ina udongo. Ardhi yenye mawe hata ukichimba bwawa hayo maji ukiyaweka baada ya kutwa moja yanakuwa yameshakauka. Lakini nitatizama kwa mule mwahala mnamoyumkinika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika asubuhi hii njema. Kwanza Mhe. Spika, kwa kuwa serikali imeamua kujenga mawizara mbali mbali na tegemeo letu ni kwamba tutahama katika yale majengo ambayo si ya kuyategemea kwa maofisi, na kwa kuwa nimshukuru sana Mhe. Waziri katika eneo la Mazizini kupatikana maji, lakini mimi na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tuna shida kidogo katika lile eneo la Mazizini kupatikana maji kwa jengo la Wizara ya Katiba na Sheria.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba ni vizuri ende akakague pale kuna wananchi wengine hawapati maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza kabla ya kumjibu napenda kutoa taarifa tu Mhe. Spika, kwamba tuna maswali mengi yanayohusu masuala ya usambazaji maji na bado yatakuja. Maswali haya yatakuwa yanapata nafasi kwa hivyo naomba sana tuzingatie kanuni ya kuuliza maswali. Swali la hapa ni suala la uvunaji wa maji ya mvua, lakini hata hivyo niko tayari kwenda kutembelea na kuona hili tatizo liliopo katika eneo alilolitaja.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Bububu kuna tatizo kubwa sana katika maeneo yote hasa shida ya maji, kama tunavyojua shida ya maji kwa binadamu ni tatizo kubwa na ni muhimu kupatikana maji. Kama katika maeneo ambayo hayapati maji kabisa ni kama Mwanyanya, Kibweni na Sharifumsa. Mimi binafsi pamoja na Chama changu cha Mapinduzi nimechukua hatua kubwa na kujitahidi kutafuta matangi 30 ya lita 5,000 ili kuipunguzia gharama wizara yako Mhe. Waziri. Je, kwa hatua hii tuliochukua sisi Chama cha Mapinduzi na mimi mwenyewe Mwakilishi wa Bububu wizara yako itatusaidia vipi kwa hatua nyengine inayofuata hapo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii mana nilikuwa sijaipata kumpongeza Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia Chama chetu cha Mapinduzi, namkaribisha sana katika Baraza hili na tutashirikiana tutafanya kazi pamoja bilashaka yoyote.

Mhe. Spika, kwa kujibu swali lake nasema tatizo la maji ni tatizo kubwa tufanyeni utaratibu wa kuwapunguzia wananchi wetu kuwapunguzia tatizo la maji kwa kuwapa taaluma ya hili suala lililoulizwa hapa la ukusanyaji wa maji ya mvua. Tuna bahatí kwamba hivi sasa nyumba zetu nyingi ni za bati, kwa hivyo maji mengi yanapukutika na kuingia katika ardhi na tungeweza kuyakusanya haya tukaweza kuyatumia kwa ajili ya kufulia, kukoshea watoto, kukoshea vyombo vyetu pamoja na mambo mengine madogo madogo tukabakisha kwenye maji ya kunywa. Na kwa sababu mvua tunazipata sana ni vizuri tujitahidi kuwafundisha wananchi wetu kuvuna maji ya mvua.

Mimi nakumbuka Mhe. Spika, tulipokuwa tuko skuli kila skuli ilikuwa inajengewa tangi kwa kutumia yale mabati ya skuli, na kwa kweli yalikuwa yakisaidia sana hata wale watoto ambao wanakuja skuli pale wamechafuka sana

basi walikuwa wakifuliwa pale pale skuli, wengine hawajakoga mwisho wa siku basi hukoshwa pale pale skuli kwa maji yale, maji humwagiliwa katika mabonde mbali mbali kwa kutumia maji yale ya mvua na hata wale ambao wana matatizo ya kepu walikoshewa maji yale yale, hivyo yalisaidia sana kupunguza matatizo hayo katika skuli zetu. Kwa hivyo, tuwafundishe wananchi wetu suala la kujipunguzia matatizo ya maji kwa kukinga maji ya mvua na kujenga mahodhi ya kukusanya maji ya mvua katika maeneo yao kutumia kwa matumizi madogo madogo itasaidia sana kupunguza hili tatizo la maji.

Lakini hata hivyo, nawambia bado wizara yangu iko tayari kushirikiana na yeye hasa kwa kuwa ameshaonesha mfano wa kukusanya hayo matangi, tuko tayari kushirikiana na yeye tutizame uwezekano wa kuweza kupata maji katika eneo lake bila ya tatizo lolote. Ahsante sana.

Nam. 49

Usajili wa Simu Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua wateja wote wa simu kusajiliwa katika kupambana na vitendo vya kutumia mitandao ya simu kwa mambo yasiofaa ikiwemo uhalifu.

(a) Je, mpango huo umesaidia kwa kiwango gani kufikiwa kwa malengo yake.

(b) Kwa kuwa vitendo vya utapeli kupitia mitandao ya simu vinaendelea kufanyika kwa kutumia namba ambazo hazijasajiliwa; Je, serikali ina mpango gani wa kudhibiti uuzaji wa "*line*" za simu bila ya kuwepo kwa kumbukumbu za wahusika katika kampuni husika.

(c) Katika kudhibiti tatizo hilo kwa nini serikali kwa kushirikiana na makampuni ya simu yasiweke utaratibu wa wateja kuuziwa "*line*" za simu baada ya kupata barua ya sheha ili kudhibiti matumizi mabaya ya mitandao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye vifungu a, b na c kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu wa usajili umefanikiwa kwa asilimia kama zifuatazo:-

1. Kwa Kampuni ya Simu ya *Vodacom* ina jumla ya wateja 8,780,620, waliosajiliwa ni watu 8,416,197 ambao sawa na asilimia 95.5 ya wateja wao.

2. Kampuni ya *Airtel* ina wateja 7,865,441, waliosajiliwa ni 7,664,413 sawa na asilimia 97.

3. Kampuni ya *Tigo* ina wateja 6,168,518, waliosajiliwa ni 6,078,066 sawa na asilimia 99.

4. Kampuni ya *Zantel* ina wateja 1,358,048, waliosajiliwa ni 1,070,000 sawa na asilimia 79.

5. Kampuni ya *TTCL* ina wateja 113,926, waliosajiliwa ni wote sawa na asilimia 100.

6. Kampuni ya *Sasatel* ina wateja 7,461 na wote wamesajiliwa asilimia mia moja.

7. Kampuni ya *Benson* ina wateja 1,680 na wote wamesajiliwa asilimia mia moja.

Mpango huu wa usajili kiujumla umefanikiwa kwa takriban asilimia 95 katika zoezi la usajili. Lakini hatua ya pili ya kukabiliana na vitendo vya uhalifu ama vya uovu zoezi hili ni endelevu na linaendelea kwa mujibu wa taratibu zilizopo za makampuni na usimamizi wa mawasiliano chini ya chombo cha Tikra.

Jibu (b) na (c) kwa pamoja Mhe. Spika, suala la usajili ni msingi wa kumuwezesha mwananchi kupata mawasiliano na katika mwaka 2010 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha sheria ya mawasiliano pamoja na *electronic* na posta kwa kifupi wanaita sheria ya *EPOCA* ambayo ilieleza adhabu pamoja na usimamizi mzuri unaolazimisha kwa mwananchi yoyote anayehitaji huduma ya simu kwenda kujisajili.

Suala la msingi ni kuona kwamba mwananchi anayekwenda kujisajili anatakiwa aache taarifa zake sahihi ili kuweza kupatikana pale anapohitajika. Lakini pia suala la kwenda na barua za sheha nalo naamini lina mazingatio makubwa katika kufanikisha utoaji wa taarifa sahihi kwa wale wanaosajili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokidhi swali la msingi naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza. Hivi sasa kumekuwa na mtiririko mkubwa wa utapeli hasa kupitia njia ya simu.

(a) Je, ni watu wangapi wameshakamatwa na kuchukuliwa hatua.
(b) Pamoja na makampuni kuvuka lengo la usajili kuna baadhi ya wateja wamekuwa wakilazimishwa kwenda kuripoti mara ya pili kupitia ujumbe wa Zantel. Je, wizara yako inachukua hatua gani kuondosha usumbufu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Samahani Mhe. Spika, hilo swali la pili sijalifahamu naomba azungumze tena taratibu namsikiliza yeye mimi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na makampuni kuvuka lengo kumekuwa na usumbufu kwa baadhi ya wateja kutumiwa *message* tena kwenda kujisajili wakati tayari wameshajisajili. Hivi juzi tu, tumo humu Barazani Zantel katuma *message* kuhusu Ramadhani wakati Ramadhani hata haijafika. Je, wizara yako inachukua hatua gani kuhusu suala hili la kuondosha usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala la utapeli kupitia katika njia ya simu nadhani hili ni suala mtambuka, wajibu wa makampuni ya simu ni kuhakikisha kwamba mtumiaji wa simu anakuwa taarifa zake, mawasiliano yake yanahakikiwa na kujulikana. Sasa kama kuna suala la utapeli kwa kupigiana simu nadhani simu itakuwa imetumika kufikisha mawasiliano lakini haikutumika katika kutapeli. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi aliyepatwa na kadhia hiyo afanye mawasiliano na vyombo husika kama chombo cha polisi na vyombo vyengine ili waendelee na uchunguzi kwa kutambua tu kwamba suala la mawasiliano ni siri kati ya kampuni na kampuni au siri kati ya mpigaji mmoja na aliyepokea, hivyo msingi mkubwa ni kushirikiana na vyombo husika ili kuweza kufuatilia kwa kadhia ili kumtambua huyo ambaye amehusika na kadhia hiyo ya utapeli kwa njia ya simu.

Lakini suala la pili kama kuna vyombo au makampuni ambayo yanapelekea usumbufu wateja wao kwa kuwakumbusha kusajili naomba tukuabaliane naye, naamini kwamba wengi wa Wazanzibari tunatumia simu kwa Kampuni ya *Zantel* na kwa mujibu wa taarifa zetu tulizokuwanazo wateja wetu wa Zantel waliojisajili ni watu asilimia 79, bado kuna asilimia 21 hawajajisajili naamini kwamba Kampuni ya Zantel inatumia nafasi hiyo kuwatafuta hawa watu asilimia 21 ili nao wajisajili kuweza kuhakikisha kwamba namba yao yote inakuwa na ukamilifu wateja wao wote watakuwa wamejisajili. Kwa hivyo, kama kuna usumbufu naomba tuendelee kuwapa ushirikiano ili na wao waweze kuitimiza hiyo nambari 21 wakamilishe usajili kwa wateja wao wote.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kusajili simu ililetwa kwa nia nzuri kwa ajili ya kuwafichua wahalifu na kujua ripoti zao, lakini pia usajili wa simu kwa nchi za wenzetu si rahisi kununua *line* kiholela ukaipata. Kwa sababu suala la uhalifu wa simu kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni mtambuka. Je, ni lini hasa serikali itaweka utaratibu mzuri ili *line* za simu zisiuzwe tu vibandani kiholela ziwe na utaratibu maalum.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri kasema kama kutumia barua za masheha ni bora zaidi lakini kuna wenzetu wageni wanaokuja hawana masheha na wakija hapa inabidi lazima watumie simu zetu kwa sababu za kwao hazifanyi kazi. Je, ni utaratibu upi watawekewa wageni na wao ili wapate simu wasisumbuke kwa masheha.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza namhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba serikali imeweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba kila mtumiaji wa simu anajisajili na utaratibu

huu ndio uliopelekea wenzetu kupitisha sheria hii ya *EPOCA* ili kwenda kusimamia vizuri na kuona jambo hili linatekelezwa kwa vitendo. Sasa mimi naamini kwamba ili ujisajili vizuri kinachotakiwa msingi wa pale ni kupeleka taarifa zako zilizosahihi.

Mfano alioutoa Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa barua za sheha alilenga moja kwa moja kwa Wazanzibari, lakini utaratibu kwa mujibu wa sheria ya *EPOCA* kinachotakiwa ni taarifa. Kwa hivyo kama kuna mgeni atakuwa mgeni huyo ameingia ana *passport* yake na tunaamini kwamba katika *passport* kutakuwa kuna taarifa zake zote zilizosahihi. Kwa hivyo, *passport* hiyo itatosha kutoa taarifa zake kwa ajili ya usajili.

Jambo jengine la msingi hapa ni kuhakikisha kwamba tunasimamia sheria yetu ipasavyo na wananchi pamoja na wateja wa makampuni wanatoa ushirikiano unaostahiki katika kufanikisha jambo hili la usajili wa simu. Adhabu zipo na kilichokuwa kinachelewa ni kwamba kulikuwa kuna kesi Mahkama Kuu wanasubiri maamuzi ya kesi hiyo ili waweze kuona namna gani sheria hiyo wanaitekeleza kwa vitendo katika usimamizi wa masuala ya usajili kwa *line* za simu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye vifungu a na b.

(a) Katika hatua ya kudhibiti uhalifu leo asubuhi nchi jirani ya Kenya imetangazwa kuwafungia wateja wake wapatao milioni tatu huduma za matumizi ya simu. Ni kwa nini Tanzania na Zanzíbar kwa jumla inashindwa kuwafungia wateja hawa ambao wamebainika na kutumia simu kama sehemu ya kufanya uhalifu.

(b) Kwa kuwa baadhi ya wananchi wanapofanyiwa vitendo vya uhalifu ikiwemo matusi hupeleka malalamiko katika makampuni ya simu na vituo vya polisi na hakuna hatua ambazo zinachukuliwa na biombo hivi. Hivyo hatuoni kwamba makampuni yenyewe ya simu yanasaidia kueneza uhalifu kwa kutokushukua hatua kwa wateja.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, sheria yetu ya *EPOCA* imetoa adhabu kwa kila mtu ambaye atakuwa hajasajili simu yake. Na kwa mujibu wa sheria hiyo mtumiani yoyote wa simu ambaye atakuwa anatumia simu yake bila ya kuisajili akibainika atatozwa faini ya shilingi milioni tatu ama kifungo cha miézi 12 jela. Na kampuni yoyote ya simu ambayo itatoa huduma kwa mtu yoyote ambaye atakuwa hajasajili kampuni hiyo itatozwa faini ya shilingi milioni 15 kwa kila mteja wao mmoja. Tunaamini kwamba sheria hii tukiisimamia vizuri itakuwa na sisi tunakwenda sambamba na hao wenzetu wa Kenya wanaowafutia wateja wao ambao watakuwa hawajajisajili. Msingi kwamba kuna tatizo la kisheria, katika utekelezaji wa sheria hii kuna mtu ambaye alilalama kesi iko Mahkama kuu. Kwa hivyo, katika utekelezaji wake wanasubiria maamuzi ya Mahkama kuu ili kuweza kuona uhalalo katika utekelezaji wa sheria husika.

Suala la Pili kama kuna mtu ambaye atakuwa amepata matusi au kadhia inayotokana na mawasiliano ya simu aidha itakuwa ni kwenda polisi, polisi ni kwenda kuwasiliana na makampuni husika ili tuweze kuona taratibu zinakwenda vizuri. Jambo la kulikumbuka ni kwamba mawasiliano ya simu ni jambo la siri si busara wala si halali kwa mujibu wa sheria ya *EPOCA* mwananchi kutendewa kosa kwenda kwenye Kampuni ya Simu kutaka apewe taarifa zile yeye mwenyewe binafsi pasina vyombo husika wakiwemo polisi na vyombo vyengine yakiwa pamoja na amri au maelekezo yaliyotoka katika Mahkama.

Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Mwakilishi kwamba, siri hizo kama zitakuwa zinadhibitiwa ni utekelezaji wa sheria na ukiwa unahitaji siri hizo unatakiwa ufuate taratibu na sheria ziliopo ili uweze kupata taarifa hizo sahihi, kwa watu sahihi na kutoka vianzo sahihi.

Nam. 56

Waandishi Kukwama Dodoma

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali langu naomba uniruhusu kuzungumza machache kwa kumpongeza Mhe. Waziri mwenye dhamana ya wizara hii kwa kuondosha muziki katika nyumba maarufu ya Ngomekongwe na nimpe salamu wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe wamefurahi sana kwa kauli ya Mhe. Waziri. Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naomba swali langu nambari 56 lijibiwe.

Kuhusu wizara hii. Vyombo vya Habari vya Serikali ya Zanzibar kwa miaka mingi sasa vimekuwa havipeleki waandishi wake kuripoti shughuli zinazofanyika Bungeni Mkoani Dodoma na kupelekea kuwanyima haki ya Kikatiba wananchi wa Zanzibar ya kupata habari.

(a) Je, sababu gani wizara imekuwa ikishindwa kuviwezesha vyombo vyake kufanya kazi ya kupasha habari za Bunge ili kuepusha wananchi kulazimika kufuatilia habari kupitia vyombo vya Tanzania Bara.

(b) Serikali lini itaanza kutuma waandishi wake na wapiga picha kufuatilia vikao vya Bunge ili wananchi wapate haki yao ya Kikatiba ya kupokea habari moja kwa moja (*LIVE*) kutoka Dodoma.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 56 lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara inapenda kuwapatia wafanyakazi wake nafasi kama hizo ili kutoa mwanya kwa waandishi wetu kupata nafasi ya kujifunza na kujionea mambo mbali mbali yatakayowapa upeo wa kazi zao hasa katika matukio muhimu ya kitaifa. Ili iwe ni sehemu ya kumpa moyo mfanyakazi na vile vile vyombo vyetu kupata habari za kila aina.

Mhe. Spika, tatizo kubwa linalotufanya tushindwe kupasha za Bunge na kuwasilisha kwa wananchi wetu wa Zanzibar ni ufinyu wa Bajeti ya Idara yetu ya *ZBC* haikidhi hata kidogo kwa safari ya Zanzibar – DSM, DSM – Dodoma. Hii inatokana na fedha zilizotengwa kwa mwaka kwa idara yetu ni shs. 8,000,000/= kwa safari zote za ndani za *ZBC*.

Serikali kupitia wizara yangu itaanza kutuma waandishi na wapiga picha kufuatia vikao vya Bunge ili wananchi kupata haki yao ya kikatiba kupokea habari moja kwa moja live kutoka Dodoma pale tu tutakapokuwa na bajeti itakayokidhi haja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kitendo cha serikali kutopeleka waandishi wa habari Dodoma huoni ni kuvunja haki ya msingi kikatiba na wananchi kutopata habari kwa maendeleo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, swali langu la msingi nimefafanua vizuri na nataka anifahamu kuwa jibu nililompa ni la ufasaha na ni la ukweli Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kuweza kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kukiruhusu kituo chetu cha televisheni kufanya kazi masaa 24 na wananchi kupata habarí za uhakika zinapotokea ajali.

Lakini swali langu ni kwamba, pamoja na kuwa bajeti yetu ni finyu je Mhe. Naibu Waziri haoni kuwa tutafute mbinu nyengine na hasa katika vitendea kazi vyetu kuwa ni vichakavu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wangu kwa namna ambavyo amejibu maswali ya msingi. Kuhusu suala hili la Mhe. Makame Mshimba Mhe. Spika, ni kweli kwamba Shirika letu la *ZBC* tuna vifaa vichakavu na sio vifaa tu lakini tunatumia teknolojia ya zamani, kama anafuatilia matukio vizuri ni kwamba juzi tulizindua kampeni kubwa katika nchi yetu ya matumizi ya teknolojia mpya ya *digital*. Sambamba na hilo ni kwamba wizara kwa kushirikiana na Shirika la *ZBC* inajitayarisha kununua vifaa vipya kwa ajili ya Studio ya *Karume House* na Studio ya Pemba ya Matangazo ya Televisheni.

Mhe. Spika, tuna imani kwamba mwanzoni kabisa mwa mwezi wa januari mwaka 2013 basi vifaa vya Studio vya *Karume House* na vya Pemba pale Mkoroshoni vitakuwa tayari vina vifaa vipya vya kisasa vinavyotumia teknolojia mpya zama ambayo itawezesha watazamaji wetu wa Zanzíbar na hata katika mwambao wa Afrika Mashariki kujionea vizuri matangazo ya televisheni yetu ya Zanzíbar.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri alitwambia kuwa bajeti yake ni ndogo je, hapo itapokamilika bajeti yake atapeleka wafanyakazi wangapi.

Mhe. Waziri wa Habarí, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, suala hili la kupasha habari katika mabunge lina pande mbili, lina upande mmoja wa vituo vya matangazo na upande wa pili ni uongozi wa Bunge lenyewe. Taarifa tuliyonayo ni kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano linailipa Shirika la Utangazaji la Tanzania *TBC* kati ya shilingi milioni mia mbili mpaka mia tano kwa kila *session* ya kikao. Sasa katika hali hiyo wizara tunashauriana na Bunge ikiwa liko tayari tulilipa Shirila letu la *ZBC* kwenda kurusha matangazo ili wananchi kuwa na pande mbili mbali ya *TBC* pia *ZBC* iweze kutoa matangazo hilo tunalifanyia kazi. Kwa hivyo ikifika hali hiyo basi Shirika la *ZBC* litapeleka waandishi wa kutosha ili kuwezesha wananchi wa Tanzania kuweza kupokea matangazo kwa kadiri inavyowezekana.

Lakini katika hali ya kujibana ya bajeti kwa kweli hilo Mhe. Spika, tutakwendanalo katika hali ngumu sana. Lakini katika hali hiyo hiyo pia naomba niseme kwamba wizara pia imeanza na mazungumzo ya chini kabisa na uongozi wa Baraza la Wawakilishi hili lako Mhe. Spika, ili matangazo haya ambayo yanatoka *live* kuanzia mwakani Baraza lianze kulipia matangazo haya kama vile ambavyo Bunge linalipia katika shirika la *TBC*. Kwa hivyo, Baraza nalo lijitayarishe tukijaaliwa mwakani wakati inatayarisha bajeti yake ione kwamba inaweka bajeti kwa ajili ya matangazo haya yanayorushwa hivi sasa basi yaweze kulipiwa katika Shirika la Utangazaji la Zanzíbar (*ZBC*) ili wananchi waweze kuyaona vizuri zaidi. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar ya 2012

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba Mswada wa Kuanzishwa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar na Mambo Mengineyo Yanayohusiana na Hayo usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika, Zanzibar nayo inatawaliwa na sheria saba zinazohusiana na biashara na mali. Sheria hizi ni pamoja na:-

1. Sheria ya Usajili wa Mali Zinazohamishika Nam. 4 ya mwaka 2011,
2. Sheria ya Usajili wa Mali Bunifu Nam. 4 ya 2008,
3. Sheria ya Jumuiya Nam. 6 ya mwaka 1995,
4. Sheria ya Usajili ya Majina ya Biashara sura ya 168 ya mwaka 1949,
5. Sheria ya Makampuni sura ya 153 ya mwaka 1952,
6. Sheria ya Uhaulishaji Mali sura ya 150 ya mwaka 1917
7. Sheria ya Usajili wa Nyaraka sura ya 99 ya 1919

Mhe. Spika, ambapo kila moja zilikuwa zinasimamiwa na Msajili wake. Matokeo yake ilikuwa hakuna utekelezaji wa pamoja na hivyo kuleta tofauti kubwa ya utaratibu wa kusajili biashara husika, ikitegemea ni wapi usajili huo unahusika kwa mujibu wa sheria hizi saba.

Mhe. Spika, madhumuni ya mswada huu basi ni kufanya suala zima la usajili yote katika sheria hizi saba uwe chini ya afisi moja ya uwakala wa usajili wa biashara na mali kwa hapa Zanzibar.

Afisi hii kwa mapendekezo yetu itaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Msaidizi wake na Naibu Msajili Dhamana kwa Pemba, itakuwa na majukumu ya kusimamia zote zinazohusiana na usajili wa biashara na mali za Zanzibar.

Lengo na madhumuni makubwa ya sheria hii basi ni kuhakikisha kuwa wakala huyo wa usajili anaimarisha uwajibikaji ndani ya afisi husika au taasisi nyengine zinazohusiana na shughuli za usajili. Vile vile Afisi itahakikisha kuwa kazi za uwakala zinafanywa na wafanyakazi wenye sifa na ujuzi watakaowajibika kwa kuzingatia sheria, taaluma, uadilifu na maadili ya kazi.

Mhe. Spika, mswada huu una vifungu 26 na umegawika katika sehemu 5.

Sehemu ya kwanza imegawika katika vifungu viwili. Kifungu cha kwanza kinaelezea jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika wakati kifungu cha pili kinatoa ufafanuzi wa maeneo kwa maneno yaliyotumiwa katika sheria hiyo.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ina jumla ya vifungu vitatu. Kifungu cha tatu kinaanzisha Wakala wa Usajili wa Biashara wa Mali Zanzibar na kifungu cha nne kinaelezea Kazi za Wakala zikiwemo utoaji wa huduma bora na usimamizi mzuri wa masuala ya usajili. Kifungu cha tano kinaruhusu kuwepo kwa matawi ya wakala katika maeneo tofauti kwa mujibu wa sheria.

Sehemu ya tatu inafafanua kuhusu uongozi wa wakala na ina jumla ya vifungu vinane. Kifungu cha sita kinaelezea kuwepo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala na sifa za uteuzi wake, wakati kifungu cha saba kinaelezea kazi za Mkurugenzi Mtendaji huyo na kifungu cha nane kinaelezea uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji.

Kifungu cha tisa kinaelezea uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji kumpa mamlaka afisa yeyote kutekeleza kazi zote au majukumu yote ya Mkurugenzi Mtendaji wakati kifungu cha kumi kinaelezea uteuzi wa Naibu Mkurugenzi Mtendaji pamoja na kuweka sifa za uteuzi. Kinaelezea pia kazi za Naibu Mkurugenzi Mtendaji na mambo mengine.

Mhe. Spika, kifungu cha kumi na moja kinaelezea uwezo wa Waziri wa kuteua Naibu Mrajis Mdhamana wa Pemba, sifa zake za uteuzi pamoja na kuelezea kazi na wajibu wake wakati kifungu cha kumi na mbili kinaelezea kuwepo kwa wasaidizi Mrajisi pamoja na kuelezea utaratibu wa uteuzi wao na kifungu cha kumi na tatu kinaelezea kuhusu uteuzi wa wakuu wa idara na vitengo na maafisa wengine wa wakala kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa shughuli hizo.

Sehemu ya nne Mhe. Spika, imeweka masharti ya fedha za wakala na ina jumla ya vifungu vinne, kuanzia kifungu cha kumi na nne hadi kumi na saba. Kifungu cha kumi na nne kinaelezea kuhusu fedha za wakala na kifungu cha kumi na tano kinaelezea mapato yaliyokusanywa kulipwa katika mfuko mkuu.

kifungu cha kumi na sita ni makadirio ya mapato na matumizi ya wakala na kifungu cha kumi na saba kinaelezea hesabu na ukaguzi wa matumizi wa wakala katika shughuli zake za usajili.

Mhe. Spika, sehemu ya tano na ya mwisho imeweka masharti mengine na ina jumla ya vifungu tisa, kuanzia kifungu cha kumi na nane hadi cha ishirini na sita. Kifungu cha kumi na nane kinaweka utaratibu wa usajili wa madaftari ya usajili wakati kifungu cha kumi na tisa kinaweka kinga ya kutokushitakiwa kwa Mkurugenzi Mtendaji na maafisa wengine wa wakala pale wanapotekeleza kazi zao kidhati. Kifungu cha ishirini kinaelezea uhalali wa nyaraka na namna nyaraka hizo zitakavyochukuliwa kuwa ni za ukweli wakati kifungu cha ishirini na moja kinaweka utaratibu wa kukabidhi raslimali, madeni pamoja na utaratibu wa watumishi ambao wameajiriwa kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii.

Kifungu cha ishirini na mbili kinaelezea kuhusu masharti na madai ambayo yalikuwa yanashughulikiwa kabla ya sheria hii na kwamba mambo hayo hayatochukuliwa kama yamo katika sheria hii na kwamba mambo hayo yatachukuliwa kama yamo katika sheria hii. Kifungu cha ishirini na tatu yanatoa makosa na adhabu, wakati kifungu cha ishirini na nne kinatoa uwezo wa Waziri kutunga kanuni zitakazosaidia ufanisi wa sheria hiyo.

Mhe. Spika, kifungu cha ishirini na tano kinaelezea kuhusu marekebisho ya baadhi ya sheria ambazo zitasaidia utekelezaji wa sheria hii, wakati kifungu cha ishirini na sita kinawahalalisha wafanyakazi wa zamani kuendelea na nafasi zao mpaka pale ambapo nafasi hiyo imeondolewa au mfanyakazi huyo amehamishwa kisheria.

Mwisho katika mswada huu una jadweli ambayo inaonesha sheria zinazohusika na sheria hii.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja na kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wachangie na waikubali iwe ni sheria. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar na Mambo Yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima na afya njema, kunipa nguvu ya kusimama mbele ya Baraza hili lako tukufu kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Kuanzishwa kwa Uwakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar inayohusiana na Mambo hayo.
Mhe. Spika, halikadhalika ninapenda nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya awali ya kutoa maoni ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya mswada huu muhimu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, aidha nimpongeze Kaimu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na watendaji wote wa wizara kwa mashirikiano makubwa waliyotupa wakati tukipitia na kuchambua mswada huu.

Mhe. Spika, kwa kuwa mswada huu wa sheria umebahatika pia kujadiliwa na wadau mbali mbali ili kusaidia kamati katika uchambuzi wa mswada husika pamoja na kuimarisha zaidi. Kamati inawashukuru wadau wote hao kwa michango yao waliyotoa.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina jumla ya Wajumbe wanane na Makatibu wawili ambao wanahusika kikamilifu katika kupitia mswada ulio mbele yetu. Naomba niwatambue na kuwataja majina kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdala	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5. Mhe. Mtumbwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
6. Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
7. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
8. Mhe. Mohamedraza Hassanali	-	Mjumbe
9. Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
10.Ndg. Abubakar Mohamed Iddi	-	Katibu

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo ninapenda sasa nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusiana na mswada kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inapongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuunda taasisi maalum inayohusika na vizazi na vifo na kuiacha Afisi ya Mrajis Mkuu kushughulikia usajili wa biashara na mali pake yake. Hatua hii ni muhimu kwani itasaidia kuondoa malalalmiko mbali mbali yaliyokuwa yakijitokeza yakiwemo ucheleweshwaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto.

Mhe. Spika, tunaunga mkono vifungu mbali mbali viliomo katika sheria sehemu ya tatu ya mswada huu. Hii ni kutokana na kuwa kitendo cha kuekea sifa za uongozi wa wakala unaashia kuondoa kabisa tabia ya kuweka watendaji kwenye taasisi kwa misingi ya kujuana. Sambamba na hilo mswada huu wa sheria umetaja majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji jambo ambalo litasaidia kuleta ufanisi zaidi katika taasisi hii.

Mhe. Spika, kamati imefurahishwa sana kwa kuanzishwa Naibu Mrajis Dhamana kisiwani Pemba. Hii ni hatua muhimu na itasaidia kuondoa usumbufu wa wafanyabiashara waliopo Pemba hasa pale mfanyakazi huyo anaposimamia vyema shughuli zake.

Mhe. Spika, baada ya kupitia mswada huu kamati yetu imependekezwa kufanyiwa kwa marekebisho kwa baadhi ya vifungu kwa lengo la kusaidia na kuimarisha mswada huu wa kisheria. Mfano wa vifungu hivyo ni kama hivi ifuatavyo.

Kwa kuwekwa rejea cross reference inayoambatana na maudhui ya vifungu halisi katika kifungu cha pili chenye ufafanuzi wa neno "Naibu Mkurugenzi Mtendaji" kwa kuwekwa kifungu cha kumi badala ya kifungu cha kumi na moja.

Aidha kwenye ufafanuzi wa neno "Mkurugenzi Mtendaji", kamati imependekeza rejea aya hiyo iwe kifungu cha sita badala ya kifungu cha saba.

Mhe. Spika, kamati imependekeza pia kufutwa kwa kifungu cha tatu cha kifungu cha saba na kwa kuwa kijifungu hiki hakijamtaja nani anayewajibika kwa kazi hiyo na kuihifadhi takwimu ya kumbukumbu pamoja na kuwa na mtiririko mzuri wa vifungu vyengine. Hivyo kijifungu kimependekezwa kiongozwe baadhi ya maneno na pia kisomeke kama kijifungu cha saba (j). Kutokana na mapendekezo hayo maelezo ya mstari wa kwanza kutoka juu ya kifungu cha 7(1) kinafutwa.

Mhe. Spika, kamati imependekeza pia baadhi ya vifungu kufanyiwa marekebisho ili tafsiri ya vifungu hivyo iendane na ile tafsiri ya mswada wa kiingereza. Kwa mfano, kifungu cha tisa kwenye maneno ya pembeni neno "kutoa" linapendekezwa lisomeke "kukasimu", kwa kuwa kwenye mswada wa kiingereza neno hilo linatumika kama *delegate*

Aidha kifungu cha ishirini chenye maneno ya pembeni, neno "halali" linapendekezwa lisomeke "uhalisia" kwa kuwa kwenye mswada wa kiingereza *authentic*.

Kwa upande wa vifungu vinavyoizungumzia adhabu mbali mbali kamati imependekeza maneno "kwenda jela", yasomeke "kutumikia kifungo". Hii ni kutokana na kuwa maneno yanayopendekezwa hapo ndio yanayotumika zaidi kwenye sheria na kanuni zetu mbali mbali.
Mhe. Spika, pamoja na hayo kamati yetu imependekeza kupunguzwa kwa muda wa uzoefu wa mtu anayeteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji na Naibu wake ili kutoa nafasi hizo zisije zikakosekana mtu wa kushika kutokana na sababu hiyo.

Mhe. Spika, kwa msingi huo ndio muhtasari wa kamati yetu kuhusiana na Mswada wa Uanzishwaji wa Wakala Usajili Biashara Mali Zanzibar. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu ili nao wauchangie mswada kwa madhumuni ya kuimarisha zaidi na hatimaye kuukubali na kuupitisha.

Mhe. Spika, ninatamka bayana kuwa mimi binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini na kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tunauunga mkono mswada huu kwa asilimia 100.

Mhe. Spika, ninashukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (Makofi).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa na tuendelee na majadiliano. Majadiliano yanaendelea. Inaonekana tumeridhika mapema sana.

Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi ya leo kuweza kuchangia na hasa ulivyokuwa mswada wenyewe umekuwa ni mzuri na aliye-*present* hapo na Waziri wetu ameleta kitaalamu umekuwa mzuri. Nawashukuru sana watu wa kamati ili kwa kuweza kutuletea sheria hii.

Mhe. Spika, sheria hii imefika wakati wake ni muafaka na kwa kweli inaweza kutusaidia sana hasa katika malengo yetu ambayo tuliyokusudia ili kuweza kufanya mambo yetu hasa hayo katika masuala ya biashara.

Mhe. Spika, ni kweli kifungu hiki ambacho mimi nakubaliana nambari moja hasa katika ukurasa huu wa 105, hii mimi ninakubaliana nayo hasa katika mswada huu au sheria ya kifungu nambari mbili isipokuwa kuna maelezo

yanahitajika vyenginevyo ni kweli hivi sasa wakati umefika kuwa neno mawakala wa biashara hasa ikifuatilia huko nyuma tulikuwa wapo mawakala, lakini inavyoonesha sheria haikwenda na wakati au ilikuwa na mapungufu.

Hivyo Mhe. Spika, mimi ninakubaliana nayo. Kwa kweli Mhe. Spika, tukizingatia masuala haya kwa mujibu wa sheria zetu hizi na mara nyingi hupenda kusema kuwa sheria zetu tunapozitunga basi ziende na wakati na hasa zitumike vile ipasavyo inavyotakiwa.

Mhe. Spika, tunatunga sheria hapa lakini hatimaye sheria hizo zinakuwa kufanya kazi kwake inakuwa ni mdogo sana. Tunakuwa tunajaribu Waheshimiwa Wawakilishi kutoa maoni yetu lakini hatimaye muda unakuwa wa kufanya kazi una-*delay time* na hasa mambo kama haya ya sheria.

Mhe. Spika, ili mimi ninataka nikwambia hasa kutokana na waziri ambalo hili suala ameliona kuwa kuleta manufaa haya ya kisheria na kuweza kutoa ufafanuzi wake na hasa kwa wale walengwa, mimi nakubaliana mswada huu kuwa sisi Wawakilishi tutaweza kuuchangia kwa mujibu wa utaratibu na kuleta ufanisi lakini unapotiwa saini tu na Mhe. Waziri basi uweze kufanyakazi.

Tukiingia ukurasa wa 106 kutokana na hii kutakuwa na afisi inayojulikana kama ni wakala wa usajili wa biashara na mali. Mhe. Spika, ni kweli huko nyuma hatukuwa na afisi aina kama hizi na hasa kwa kweli kutakuwa na malalamiko ya wananchi kutokana na hasa bidhaa zetu ambazo zinazoingia, kwa kweli tulikuwa ni watu ambao hajui twende tukashitakie wapi.

Lakini leo kifungu hiki kinatwambia kuwa kutakuwepo na afisi inayojulikana kuwa ni wakala wa usajili ambao hawa wasajili nao wajielewe nao kuwa watakuwa na majukumu makubwa sana. Katika usajili wao waangalie hasa vigezo kwa sababu wakala wengine wanakuwa ni watu ambao ni boshani tu; tuseme kitu kama hicho, wanakuwa wanadanganya hata zile *CV* zao za kuonesha ya ufanisi wa kuleta biashara zenyewe zinakuwa hafifu.

Lakini kwa kuwa kasikia kuwa kuna kitu kunasajili basi mtu hujitokeza na akenda, na hasa katika masuala ya kampuni ninaomba sana hapa Mhe. Spika, na hawa makampuni wetu ambao idara husika tuangalie hivi makampuni zinakuwa nyingi kama uyoga lakini ukiangalia mantiki yake kampuni zile zinazosajiwa kwa kweli hazileti mantiki. Mimi niseme ni kampuni *Briefcase Company*.

Sasa hii Mhe. Spika, itakuwa hatwendi na taalum iliyokuwa ni nzuri ambayo yenye kuleta ufanisi hasa katika mfumo huu wa sheria tuliyokuwa tunao tunaotaka kuuleta hapa.

Mhe. Spika: Mhe. Thuwayba tusubiri kidogo ninaona, hebu tulia kidogo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, tukenda katika ukurasa huu huu kifungu nambari nne na nambari moja, Wakala atahakikisha ubora na ufanisi wa kusimamia utekelezaji, sheria zinazohusiana na usajili wa biashara, mali kama ilivyoainishwa ndani ya jadweli ya sheria hii na kuwezeshwa kufanyiwa marekebisho na waziri wakati wowote.

Mimi Mhe. Spika, kifungu hiki ninakubaliana nacho na wala sina tatizo nacho. Mkazisho wangu Mhe. Spika, hapa hii *topic* iliyokuwemo humu basi ninaomba sana kuwa iendelee hivi hivi na ufanisi wake uendelee vizuri. Lakini tunaandika vizuri lakini hatimaye usimamizi wetu unakuwa ni mbovu.

Mhe. Spika, kwa kuwa sasa hivi ninashukuru sana kuwa juzi tu walipata semina wa watendaji aliyotoa Mhe. Rais; kwanza hapa ninamshukuru sana Mhe. Rais kwa kuwapa taaluma mawaziri na watendaji wetu wakuu. Nina imani kubwa kuwa sasa sheria tunazozipitisha hapa Mhe. Spika, zitafanya kazi kwa ufanisi, kwa sababu ilionekana huko nyuma na tukitizama kuna mambo ambayo tunayapitisha unakuwa ni urasimu mkubwa sana.

Sasa mimi juzi tu niliposikia Mhe. Rais ametafuta fedha za kuwaelimisha mawaziri na watendaji wake, hiyo moja imetupa faraja hasa mimi imenipa faraja nikiwa ni mmoja katika *backbenchers* kuwa sasa ni ufanisi kwa sababu tatizo letu la mawizarani Mhe. Spika, tunachelewa tunaurasimu wa kupitisha ile *process* inayotakiwa.

Inavyotakiwa mtu akileta lile ombi la kufanyiwa registration basi mimi ninafikiria mzungu tusimzungushe, tumechelewa basi ni *one week* yule mtu iwe tayari ameshaweza kupata ile hati inayohusika kwa mujibu wa sheria. Lakini itakuwa na urasimu.

Mhe. Spika, watu wanakuja kutaka kufanya *registration* wanachukua muda mrefu mpaka mtu anaamua leo analokusudia kutaka kulifanya hapa Zanzibar linaondoka. Sasa nalo hili niseme kuwa nimefarajika sana kwa mheshimiwa wetu, mpenzi Mhe. Dr. Shein kwa kuliona hili na kuweza kufanyikisha.

Mhe. Spika, nikishuka chini kidogo katika kwenye ukurasa huu wa pili kutokana na masharti ya kifungu hiki, waziri anaweza kuchapisha katika gazeti la rekebisho na kuweka upya jadweli lililoelezwa cha kifungu hiki katika utekelezaji wake wa kazi wakala na kusimamia mambo yafuatayo, kutoa huduma bora, ufanisi kwa wateja na jamii kwa jumla.

Mhe. Spika, hapa ndipo penye haja. Ninakubaliana nayo sentensi hii lakini kukubaliana kwangu kutakuwa namna hii. Hii kauli Mhe. Spika, itakuwa kwenye *Hansard*.

Kifungu hiki mimi nitakubali kipitishwe lakini kitakapokuja kikageuka kikawa hakina ufanisi ambao unaotangazwa hapa au tunaousema hapa Mhe. Spika, hilo mimi sitoingia dhambini, litafutika kwa nia yangu *automatically* litajifuta kwa sababu ukweli tuuseme ni hivyo.

Ninapitisha Mhe. Spika, kwa nia nzuri kwa sababu lililosemwa humu kuwa kutafanyika ufanisi mzuri sana na hasa kutokana na jamii, ndio lengo letu kuwasaidia katika masuala yao, hilo ndio lengo kubwa ndio maana waliotuleta hapa Barazani kwa sababu hiyo.

Sasa Mhe. Spika, hatukuwafanyia ufanisi mzuri tutakuwa hatuwafanyii haki. Mimi ninachosema kuwa tusiwe wajuzi wa kuandika ripoti hizi lakini tuwe na watekelezaji, kwa sababu utekelezaji unakuwa ni mgumu kabisa Mhe. Spika, na hiyo ndio maana siku zote wananchi wanazidi kupata taabu na kudhalilika.

Sasa mimi ninaomba Mhe. Spika, sheria hizi tunapozipitisha Mhe. Spika, basi ziende na yale matakwa hasa tuliyokusudia, tusiripue tu hapa, tusiwahangaishe wanasheria wetu au wataalamu wetu. Hilo mimi Mhe. Spika, ninakubaliana nalo kabisa bila ya tatizo lolote.

Lakini nikishuka chini kwenye kifungu cha tano, wakala inawezekana akawa na matawi ya afisi itakazosaidia utekelezaji mzuri wa kazi au kama itakavyohitajika kwa mujibu wa sheria ninakubaliana nalo.

Mhe. Spika, hiyo ni moja katika kuondoa urasimu, tukiwa na matawi itasaidia sana na sio watu wote ambao watakwenda katika *head office*. Hii niseme kuwa hata na afisi nyengine wenye kuwa na mambo kama haya kuwasaidia jamii tuwapunguzie adhabu wananchi wetu, wengine ni maskini ya Mungu hawana fedha ya kufika kwenye matawi kwenda kujua au utaratibu unavyotakiwa, inabidi sasa pakiwepo na matawi basi Mhe. Spika, kutakuwa na fanisi mzuri wa kuweza kufanya kazi nzuri.

Mhe. Spika: Wajumbe wanaonyoosha miguu pale njee kwa dakika chache naomba warudi ili tumalize kazi.

Mhe. Makama Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ukurasa huo huo 106 kifungu cha 6(1) “Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji Wakala atakayeteuliwa. Sifa atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mkurugenzi mtendaji huyu iwapo ni Mzanzibari na shahada ya sheria ya uongozi inayohusiana na hivyo kutoka katika Chuo kinachotambulika na uzoefu”.

Mimi naomba Mhe. Spika, niongeze hapa pamoja na sifa hizo basi na shahada ya biashara pia awe nayo. Hiyo mimi naomba tuongezee katika kifungu hiki kuwepo pamoja na uzoefu, ninakubaliana uzoefu unamsaidia mtu, uzoefu ni taaluma, sio lazima uwe na cheti cha *diploma* au *certificate* au nini, lakini Mhe. Spika, uzoefu ni taaluma. Tukiangalia sisi wengine *experience* yetu kama mimi nikwambia *experience* yangu mimi, basi ni sawa sawa na mtu wa PhD, pengine mtu wa PhD ninaweza nikamshinda kabisa, tena nina imani hiyo na sina jokes ninakwambia ukweli kwa sababu tayari akili yangu inakuja nini ninachofanya, hiyo peke yake ni *certificate*.

Mhe. Spika, akili yako ukijua nini unachokifanya basi tayari automatically umeshakwenda skuli na tayari umeshapata vyeti vya aina hiyo niliyoisema. Sasa hii Mhe. Spika, ninaomba sana hapa taaluma hii nayo huyu mtu wa biashara lazima aongezewe awe na certificate ya kuonesha kama na diploma ya kibiashara hapa ili alete ufanisi mzuri aweze kushughulikia vizuri, vyenginevyo vyovyote tu Mhe. Spika, hiyo mimi nitakuwa sikubaliani nalo.

Lakini Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapokuja kunijibu akubaliane na hilo kuwa tunaongeza ufanisi ili mtu huyu tumuongeze aweze kufanyakazi zake vizuri na ile *experience* yake ni jambo kama hili awe nalo mule na utendaji wa biashara jee amefanya, anayo *certificate* hiyo.

Mhe. Spika, nikiendelea tena hapa kwa kushuka chini niende katika ukurasa huu wa 107 ili tena ninataka nimalizie ili niweze kuwapitisha wenzangu. Ninakwenda kwenye nambari saba "Bila ya kuathiri matumizi ya kifungu cha 7(3) cha sheria Mkurugenzi Mtendaji atakuwa na kazi zifuatazo, kufanya kazi za usajili kwa mujibu wa sheria zinazohusiana". Mimi ninakubaliana nacho kifungu hiki asiingilie kazi nyengine na hii ndio tabia yetu mkurugenzi anaweza kazi yake ile inayokubalika basi anaweza akamfanya yule mfanyakazi wake kumuingilia katika masuala ya kazi. Nalo hili Mhe. Spika, sina tatizo nalo lakini akumbuke tu nini anachofanya.

Kuweka kumbukumbu za usajili daftari au takwimu Mhe. Spika, ni kweli ni wachache sana wizara ambazo zenye takwimu ya mambo yao, na hii ndio inakuja ni athari kubwa. Utakuta Mhe. Spika, sometimes tunawauliza maswali mawaziri anakwambia nitakuletea kwa maandishi kwa jambo fulani lina *cost* au bei au wingi, sasa hii ingekuwa mtu kama yule anazo data kama hizi, uwekaji wa kumbukumbu, sidhani kama ingekuwa ni suala ambalo Mhe. Spika, lichukue muda la kuweza kujibiwa la mawaziri wetu au kuletewa watendaji kupitia kwa mawaziri.

Mimi hapa nina wasi wasi mmoja Mhe. Spika, watendaji wanapokuwa wanafanya registration basi inavyoonesha hawawapelekei mawaziri au hawapelekei wale wakurugenzi wanaohusika. Ndio maana inafika hitilafu hapa Mhe. Spika, kuwa inapofika pahala anapoulizwa swali waziri anakuwa hana la kusema, anakwambia nitakuletea kwa maandishi baadae, lakini haliji tena lile, ndio imetoka hiyo.

Sasa nalo hili ningeomba sana Mhe. Spika, usajili huu twende vizuri na tukubaliane nao. Lakini kifungu cha;

> (c) Kutoa taarifa ambazo zinahusiana na usajili kwa mujibu wa sheria zinazohusiana. Tunakubaliana kwamba kila mtakapoweza kutoa taarifa zile kwa wale walengwa, basi inatusaidia na tunakuwa na kumbukumbu nzuri na watu wanafahamu. Sasa nayo hii tabia ya kufanya hivyo.
>
> (d) Kukusanya na kuwajibika mapato yote kwa mujibu wa sheria zinazohusiana. Hapa ndio mtihani.
>
> Mhe. Spika, tunakusanya na kuwajibika. Maana yake tukusanye, kuwajibika kwetu Mhe. Spika, tusimamie mapato yetu ili yaingizwe serikalini. Hapa ndipo mara nyingi uangalifu wetu unapokuwa mdogo sana, ndio maana tunafika pahala tunatoa *data* za ukusanyaji zinakuwa hafifu, sio za kweli na hatimaye tunaichanganya hii bajeti yetu, tunazungumza kuwaambia wananchi wetu masuala ya bajeti, kwamba uchumi unakua, na ndio maana uchumi katika *level* ya juu. Haukui uchumi kufika katika lengo la *grassroots* ambapo hawa wananchi tunakubaliana nao ambao wametuweka hapa.
>
> Kwa hivyo, mimi nakubaliana na kifungu hiki kwamba tuwajibike, tusimamie ipasavyo. Haya makusanyo yetu ya kodi tusimamie ipasavyo, kwa sababu tunapoisimamia tunaleta uchumi wetu wa hali ya juu. Mimi zamani Mhe. Spika, nikiona serikali imenunua magari mazuri makubwa, basi mimi nasema ndio, uchumi umekua. Lakini sio hivyo. Mimi nikijiangalia wakati ule niko mitaani sina kazi, ndio hiyo hitilafu yenyewe inavyokuja, uchumi ukikua na mimi nipate kazi, ndio lengo lenyewe.
>
> Lakini mimi ninavyoona Mhe. Spika, kwamba ni lazima hapo tuweze kuwajibika katika suala hili la kusimamia vizuri, mapato yaingie serikalini.
>
> (e) Kutoa ushauri wa serikali kuhusiana na masuala ya utoaji wa hudma, usajili na biashara amali, kwa mujibu wa sheria zinazohusiana. Mimi nakubaliana na kifungu hiki. Mhe. Spika, serikali lazima sasa hivi ipewe ushauri na ikubali ushauri ule inayopewa, hasa kwa jamii, waende huko chini wakafuate ushauri, halafu baadae ndio iende kwa wahusika waende katika *level* ya serikali kuipa ushauri.

Mhe. Spika, sasa hivi biashara tunazielewa nyengine zinakuja zilizokuwa sio nzuri, tunakula vyakula vilivyokuwa vibovu kutokana na sheria zetu zilizokuwa hazina nguvu. Kama sheria zipo basi ule usimamizi wake unakuwa ni mdogo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa vile na wenzangu nao wanataka kuchangia, basi mimi nifikie hapa. Mhe. Spika, kila nikitaka kusita naambiwa niendelee. Baniani kasema, jumba jumba ya maneno, mimi kusema kwangu sio tatizo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naendelea.

Mhe. Spika: Kama unayo maneno ya kusema lakini, kama huna basi ukae tu. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Spika, mimi nikushukuru kwa maelezo yako sasa hivi, mimi nayaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, na mimi nishukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia angalau kidogo katika mswada huu muhimu.

Mhe. Spika, mswada huu wa uanzishwaji wa chombo hiki

Mhe. Spika: Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, pamoja na kwamba umeshamaliza kuchangia, ningekuomba ukabaki ili tukamaliza kazi hii.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, mswada huu wa uanzishwaji wa chombo hiki, umekuja baada ya juzi kupitisha mswada muhimu wa sheria unaohusiana na masuala haya. Katika hivyo Mhe. Spika, suala la umuhimu wa biashara katika uchumi wetu kwa kweli hakuna asiyejua, kwamba Zanzibar katika mapato yake inategemea zaidi katika biashara. Tatizo kubwa lililojitokeza zaidi katika miaka ya karibuni ni kuwa na wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa, kitu ambacho ni dhahiri kwamba kinatupotezea kodi nyingi zitokanazo na biashara. Bahati mbaya zaidi kwamba na hata serikali nayo ni wakati mwingi hufanya biashara, kwa sababu serikali kwa upande mwengine inafanya biashara au inashirikiana na wafanyabiashara. Serikali wakati mwingi hushirikiana na wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa, hawakusajiliwa hata katika mambo ya ulipaji kodi katika mamlaka zinazohusika, kitu ambacho kwa kiasi kikubwa sana hupelekea serikali kuingia hasara na kushindwa kukusanya fedha nyingi zitokanazo na kodi itokanayo na biashara.

Kwa hivyo, kwa vyovyote vile niipongeze serikali kwa hatua hii ya kuanzisha chombo hiki ambacho kitasimamia na kuwasajili wafanyabiashara wote wakubwa na hata wale wadogo. Mhe. Spika, kama ilivyosemwa juzi kwamba mambo yakikaa sawa hayana ulazima wa kuyachangia, tukubali kupitisha. Maana yake sio lazima kuchangia kitu ambacho kiko safi. Tukifika pahala tukiona kwamba sheria iko safi, basi ni wajibu wetu kama Baraza kuipitisha na ni wajibu wetu kwa kweli kuitolea baraka. Kwa sababu juzi tuliliogelea zaidi katika eneo hili, kwa hivyo leo maneno yatakuwa ni machache sana.

Sasa Mhe. Spika, madhumuni ni kama yalivyoelezwa kwamba madhumuni makubwa ya mswada huu ni kurasimisha usajili wa biashara inayomilikiwa na ama mtu mmoja mmoja, kikundi ama kampuni. Kwa hivyo, hilo lengo ni zuri na utawala wa chombo hiki umepangika vizuri, kutakuwa na Mkurugenzi ambaye sifa zake zimetajwa vizuri katika kifungu cha 8.

Vile vile Mkurugenzi atakuwa na Naibu Mkurugenzi Mtendaji kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 10 pamoja na uwezo wao katika mambo ya utawala. Katika kifungu cha 10 hicho, mbali ya sifa ambazo zimeelezwa katika kifungu cha 10(b), ana Shahada ya Sheria au Uongozi au inayohusiana na hizo kutoka katika Chuo Kikuu kinachotambulika.

Mhe. Spika, ni muhimu zaidi kwa mtu huyo, ni lazima awe na sheria lakini inayohusiana na mambo ya biashara, abobee katika suala zima linalohusiana na biashara, isiwe ni sheria tu ya kawaida. Lakini napendekeza iwe ni sheria au utawala unaohusiana, yaani ujikite zaidi kwenye fani ya biashara. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri ataweza kufanya masahihisho hayo au aliongezee hilo katika sheria, na mambo mengine nadhani Mhe. Spika, yamekamilika.

Mhe. Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chake Chake, tunadhani kwamba sheria hii itakapopitishwa na ikatekelezwa, maana yake sio kupitishwa tu na ikatekelezwa, kwa kuwasajili wafanyabiashara wote naamini kwamba serikali hata suala lile la ukwepaji wa kodi zitokanazo na biashara, basi itakuwa imepata muarubaini wake. Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi).*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo sana kwenye mswada huu ambao Mhe. Waziri hivi asubuhi ameuwasilisha, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani.

Mhe. Spika, nianze kwa kusema yale maneno aliyosema Mhe. Omar Ali Shehe, kwamba jambo likiwa zuri huna haja ya kulitia maneno, lakini naomba nizungumze mambo machache sana kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri au kumkumbusha mambo yafuatayo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 6 kwenye mswada huu wa Mhe. Waziri unasema kwamba kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala, ambaye atateuliwa na Mhe. Rais.

Mhe. Spika, sifa za Mkurugenzi huyu ambazo Mhe. Waziri amezipendekeza kwenye mswada huu. Ya kwanza ni kwamba lazima awe Mzanzibari. Mimi nataka nimtahadharishe Mhe. Waziri, kuhusu huyu Mkurugenzi ambaye anaambiwa atakuwa na sifa ya Uzanzibari. Uzanzibari maana yake ama atakuwa ameomba au tuseme atakuwa amezaliwa. Kama itakuwa ni kuzaliwa, maana yake atakuwa na cheti cha kuzaliwa ambacho kimetolewa na ofisi ya Mhe. Waziri, Ofisi ya Vizazi na Vifo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nimejenga khofu kwamba kadiri ambavyo tunawatetea Wazanzibari, lakini kumekuwa na Wazanzibari ambao wanalazimisha kuwa Wazanzibari. Kwa maana ya kwamba ofisi yake Mhe. Waziri inashutumiwa kwa kutoa vyeti vya kuzaliwa vya watu ambao sio Wazanzibari, lakini wanajiita Wazanzibari. Sasa iwapo mtu aliyepewa cheti cha kuzaliwa cha kughushi, kwa maana kwamba yeye analazimisha kuwa Mzanzibari na hatimaye akapewa sifa ya kuwa Mzanzibari, na hatimaye huyu anakuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa sheria hii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba Mhe. Waziri anitoe wasi wasi na anitoe wasi wasi kwa msingi mmoja tu, kwamba vipi atafuta vile vyeti ambavyo vimebainika kuwa ni vyeti feki, vilitolewa kwa watu ambao sio Wazanzibari kwa ajili ya kujipatia haki za Wazanzibari, kama walivyo Wazanzibari halisi.

Mhe. Spika, nasema hayo kwa sababu kuna ushahidi mbali mbali ambao kuna watu ambao sio waaminifu hapa Zanzibar wanajaribu kughushi vyeti vya kuzaliwa na kuwapa watu waliokuwa sio Wazanzibari na kujiita Wazanzibari. Hawa ndio baadae wafanyakazi wetu na bila shaka hawa baadae watakuwa ni Marais wetu, kwa sababu ukishakuwa na ushahidi kwamba wewe ni Mzanzibari, basi utapewa haki zile ambazo Mzanzibari anastahiki.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri anitosheleze ni vipi atadhibiti wimbi hili la kutoa vyeti vya bandia au vyeti feki au vyeti vya kughushi na kuwapa watu ambao sio Wazanzibari na wakapewa haki hii ya msingi ya Mzanzibari, kwa ajili ya kutunyima haki zetu kama Wazanzibari.
Mhe. Spika, sambamba na hilo tumeona kwamba sasa watu walio wajanja wanadiriki hata kughushi vyeti vya ndoa kwamba yeye amemuoa Mzanzibari, lakini ukimfuatilia Mzanzibari yule sio Mzanzibari ni jina tu, sio Mzanzibari halisi, lakini amejipatia chetu cha kuzaliwa kwa maana kuwa yeye ni Mzanzibari, jambo ambalo kwa kweli sio haki Wazanzibari hatuwafanyii haki katika suala hilo.

Mhe. Spika, sheria hii ni nzuri, lakini iwapo sifa za Wazanzibari zitazingatiwa kwa mujibu wa sheria na iwapo hakuna mtu atakayeghushi sifa Mzanzibari akajipatia haki ya Kizanzibari. Sasa Mhe. Waziri namuomba sana anipe maelezo ya kutosha kwa ajili ya kifungu hiki, vipi atawadhibiti wahalifu hawa ambao wanatuingilia katika mifumo yetu ya haki, kwa ajili ya kujipatia haki ambazo sio zao, kwa ajili ya kujipatia mambo ambayo hawastahiki kupatiwa.

Mhe. Spika, niungane na wenzangu kwamba biashara hizi ni lazima zisajiliwe na zisajiliwe, na zisajiliwe biashara ambazo ni kubwa kubwa na biashara ambazo ni ndogo ndogo, kwa ajili tu ya kupata uhalali, lakini pia kudhibiti mapato ya serikali kama nyenzo kuu ya kuiendesha nchi yetu.

Vile vile Mhe. Spika, nimshauri Mhe. Waziri kwamba wakati wa utungaji wa kanuni, lazima azingatie ile mianya ambayo wahalifu wanaweza wakapenya, ili kukwepesha mapato ya nchi na kudanganya sekta nzima hii ya biashara, kwa ajili ya kutoa uhalisia wa biashara wanazozifanya.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nimuombe Mhe. Waziri kwamba aendelee kuwadhibiti wafanyakazi wa ofisi yake ili wasishiriki katika vitendo vya kihalifu vya kuwapatia waliokuwa sio Wazanzibari vyeti vya kuzaliwa na vyeti vya ndoa kwa ajili ya ufanisi wa taifa hili.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuunga mkono mswada huu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache katika mswada huu.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku ya leo kuweza kuwa salama na tukaweza kuendelea na shughuli zetu katika ukumbi huu. Pia nichukue fursa hii vile vile kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kutokana na kazi nzuri ambao wameifanya hata sisi tukashindwa kutafuta eneo hasa la kuweza kutia makosa, kutokana na kazi nzuri ambayo wenzetu wamekwishajitahidi kuifanya.

Lakini pamoja na yote hayo Mhe. Spika, mimi nilikuwa na tatizo kidogo katika ukurasa wa 106 katika sifa za uongozi hapa. Mhe. Spika, katika kifungu cha 6(c), ambapo mara nyingi sana katika miswada ambayo ilikuwa imepita, tulikuwa tunazungumzia suala la sifa ya uongozi, ukurasa wa 106 na 107. Kuna sifa nambari (c) ambayo inasema kwamba yule mtu ambaye atakuwa na haki ya kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji, awe na sifa (a) Mzanzibari. Mimi sina tatizo na Uzanzibari. (b) Awe na Shahada ya Sheria au Uongozi sina matatizo nayo. Lakini sifa ya kwamba awe na uzoefu wa kazi katika eneo hilo usiopungua miaka 7. Hapa ndipo penye tatizo na mimi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano tunatumia fedha nyingi sana kusomesha vijana wetu ili waweze kuingia katika soko la ajira. Vijana hawa wanapomaliza masomo huwa hawana ujuzi kama huu ambao unaainishwa katika miswada hii ya kisheria ambayo tunakuwa tunaipitisha hapa. Tunapowawekea vipengele au vigezo hivi vya kwamba lazima upatikane uzoefu wa miaka 7, wimbi la vijana ambao tayari wako nje wanatafuta ajira, maisha yetu yote tutakuwa vijana hawa hatuwatendei haki na wala hatuna uwezo wa kuwaajiri. Kwa sababu uwezo ule wa uzoefu wa miaka 7 au miaka 5 ambayo inakuwa inatakiwa mara nyingi, huwa wao hawana. Lakini wanao uwezo wa kitaaluma katika utaratibu kama huo wa shahada zao na mambo mengine na wamepitia kozi mbali mbali, na tutakapoweza kuwachukua tukawaweka katika *field* kwenda kufanya kazi basi wanaweza wakafanya kazi vizuri sana. Lakini ukiangalia kwenye hizi sifa za kuweza kuteuliwa na kuwekwa katika nafasi kama hizi wanakuwa hawana. Moja ikiwa hii ya uzoefu wa miaka 7.

Kwa hivyo, ningeomba sana, tunapopitisha miswada yetu basi tuangalie kwa vizuri sana na wimbi lile la vijana ambao tunawasomesha, wapo kwa wingi nje na ambao wana uwezo, tatizo lao kubwa ni huu uzoefu wa miaka ambayo inaainishwa katika sheria zetu na hizi ni sheria. Zinapokuwa zinapitishwa hizi sheria na wale wakawa na sifa nyengine zote, ya kwanza na ya pili wanayo, sifa ya tatu ikiwa hawana basi wimbi hili la vijana litaendelea kubakia nje na itakuwa haliwezi kuajiriwa katika taasisi za kiserikali na maeneo mengine.

Kwa hivyo, mimi ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja kipengele hiki tukiangalie tena ili tuende sambamba na uhalisia wa vijana ambao wengi wako nje na wanahitaji ajira katika nchi yao. Kama hatukuweza kuwasaidia vijana wetu katika nchi yetu, basi tusitegemee kuwa nje wanaweza kupata msaada kama huu. Baada ya maelezo hayo kama Waziri atakapokuja hapa akanipa maelezo ya kunitosheleza na kuweza kukifanyia ukarabati kipengele hiki na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia kadhaa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kupata fursa ya kuchangia mswada huu uliopo mbele yetu, angalau maneno mawili au matatu.

Mhe. Spika, ni lazima tukiri kwamba Mhe. Waziri amejitahidi kwa mswada huu, ndio maana Wajumbe wako unaona wanashindwa hata kuchangia, kwa sababu mswada ni mzuri na umekamilika, hata mtu anavyojitahidi vipi

kuuangalia basi kile cha kutia nyama inakuwa kidogo ni tabu. Kwa hivyo tumsifu Mhe. Waziri kuwa amejitahidi pamoja na watendaji wake.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumzie, kama nilivyokuambia Mhe. Spika, kwamba huwezi kupata hata pahala pa kutia nyama, lakini wakati sisi ni kazi yetu ni lazima tuzungumze japo kidogo.

Mhe. Spika, pamoja na kumsifu Mhe. Waziri, lakini serikali imeona kama kuna umuhimu wa kusajili hizi mali au hawa mawakala wetu kwa ajili ya biashara zetu zilizopo Zanzibar. Sasa mimi niseme tu kama Watanzania tuna tabia nzuri sana ya kutunga sheria zetu vizuri, lakini utekelezaji wake unakuwa unasuasua. Kwa hivyo, mimi nimuombe Mhe. Waziri wakati sheria hii tutakapoipitisha basi yeye Waziri aone kwamba sasa atakuwa msimamizi mzuri wa sheria hii kufanyakazi kwa ajili ya usajili wa hizo biashara zetu zilizopo Zanzibar.

Lakini wakati huo huo Mhe. Spika, ni lazima tunapofanya usajili basi tufanye usajili na tufanye kiwango ambacho tutakuwa tunawahurumia wale wafanyabiashara wetu, isiwe badala ya kuwa tunafanya wema ikawa sasa tunawakomoa wafanyabiashara. Kwa hivyo, tusajili lakini tuweke kiwango ambacho kitakuwa kinalenga kutokana na ile biashara ya mtu anayoifanya.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni kwamba tukishasajili mali zetu basi tuone kama vile viwango tunavyoweka basi vinaenda sambamba na tuwe wakaguzi wa kuziangalia na tuwe na muda maalum wa kuzikagua. Isiwe baada ya kwishakusajili basi ndio tumeshasajili tu ndio moja kwa moja, kuwe na muda maalum wa kupitia na kuangalia kama utaratibu gani unakwenda wa kujua zile mali zetu.

Mhe. Spika, kama nilivyokuambia kuwa huu mswada ni mzuri, hatuna cha kusema kwa sababu ya uzuri wake, lakini almuradi kwa sababu ni kazi yetu, basi na sisi kidogo tutie nyama ili Waziri aone kuwa mswada wake tumeukubali.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, baada ya hayo machache, mimi naunga mkono kwa asilimia mia juu ya mia wala sina pingamizi. Ahsante.
Mhe. Spika: Mnajua kutumia chombo hiki, halafu ukabadilisha vyengine inakuwa ni tatizo. Lakini kwa kuwa muda upo na kanuni zinaruhusu hivyo, wengine wamejitokeza na naomba tusiwaache, kwa kuwa watakuwa na maneno mawili matatu basi na wao tuwasikilize. Mhe. Saleh Nassor Juma, baadae Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Inaonekana bado jengo lina *echo*, kwa sababu anatajwa Mhe. Saleh Nassor, ananyanyuka Mhe. Fatma Mbarouk, hili ni tatizo. *(Makofi/Vicheko).*

Lina *echo* bado jengo lako Mhe. Spika, kwa hivyo nadhani iko haja.

Mhe. Spika: Halikuwa tatizo la *echo*, alifikiri hakuna wengine, unajua nilikuwa ninawatafuta sana, sasa ndio maana Mhe. Fatma Mbarouk na yeye akasimama. Mhe. Saleh Nassor endelea.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kuweza kutuamsha leo tukiwa wazima wa afya na hatimaye kutupa nguvu na uwezo wa kuondoka katika maeneo yetu mpaka katika jumba hili la kutunga sheria. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Nadhani kabla sijaanza mchango wangu Mhe. Spika, nitakuwa sikukutendea haki na wewe kutokushukuru kwa kunipatia nafasi ya kutoa maneno kidogo katika hii hoja iliopo mbele yetu. Baada ya hayo Mhe. Spika, nadhani sasa niende kwenye huu mswada wa Uanzishwaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar.

Mhe. Spika, kama kuna tatizo ambalo tunalipata wanasiasa ni pale Mhe. Waziri anapoamua kutuwekea mawaziri katika wizara wakiwa na zile *profession* ni tatizo kubwa kwetu sisi, kwa sababu hatupati kuwasema sana. Tunapata tatizo la kuwa hatupati kuwasema.

Kwa mfano, huyu Mhe. Abubakar Khamis Bakary yeye ni Mwanasheria halafu kawekwa katika mambo haya, inabidi uwezo wa kumkosoa sisi ni tatizo. Lakini pamoja na hayo, kwa sababu haya mambo ya kusema maneno wengine tumesomea, basi naomba kidogo nianze na hapo kwamba uanzishwaji wa hii biashara na uhalali hapa Zanzibar.

Kwa kweli Mhe. Spika, kwanza napenda niishukuru serikali yetu kwa kuweza kuuleta mswada huu, mswada huu utakuwa ni mkombozi, sio tu kuwa utainua biashara na uhalali wa biashara katika nchi, lakini vile vile tuna wasi wasi kwamba kuna mali katika nchi hizi ni chafu, kuna mali chafu Mhe. Spika. Juzi tu hapa nilisema kwamba unamuona mfanyabiashara ana biashara yake anapitanayo kwenye *briefcase*. Huyu anasafiri na *briefcase* ndio anakwenda kwenye biashara, lakini anaporudi fedha zinakuja kwa makontena, yaani fedha zinakuwa nyingi zaidi kuliko ile biashara. Sasa nadhani mswada huu utaangalia biashara za aina hii.

Mhe. Spika, kuna makampuni hapa. Mimi mwenyewe binafsi katika miaka ya 1970 kutokana na njaa, nilianzisha kampuni. Mimi ni mwalimu *in profession*, lakini nilikuwa najenga. na ni *architecture* sijasomea hata siku moja mambo hayo. Pia ofisi yangu ilikuwa ni mkoba wa ukili na nilikuwa napewa *tender* za kujenga, kutokana na njaa napewa *tender* najenga. Sasa tatizo ilikuwa hao wanaonipa kazi zao watanipata wapi kama mimi nikikimbia. Kwa sababu sina ofisi wala *profession* ya *contractors*. Kwa hivyo, kampuni kama hizi zipo Mhe. Spika. Kwa hivyo, mimi nadhani mswada huu Waheshimiwa Wajumbe tukiupitisha hapa na Mhe. Rais akiusaini kuwa sheria, basi naamini vijikampuni kama kile kijikampuni changu nilichokuwanacho, kijikampuni uchwara havitasajiliwa. Kampuni zitakwenda na vigezo.

Kwa hivyo, nasema Mhe. Spika, sina sababu yoyote ya kuukataa huu mswada, kwa sababu naamini sio tu utaleta ufanisi na utendaji katika nchi, lakini vile vile unaweza ukaziona biashara zile ambazo ni ndogo lakini fedha ni nyingi wanaweza wakaangalia huko.

Mhe. Spika, tatizo jengine ambalo kabla sheria hii kuwepo ni tatizo la kuzungushwa zungushwa. Kipindi kile mimi nataka kufanya usajili na ile kampuni yangu sitaki niitaje, lakini wakati huo natafuta usajili na hiyo kampuni yangu, ilikuwa ni *briefcase company*, nilikuwa nahangaika huku na huku mpaka nikauza ng'ombe wanne madume. Nilikuwa sipati kusajiliwa, lakini baada ya kuuza ng'ombe kampuni yangu ilisajiliwa Mhe. Spika. Ng'ombe wanne niliwauza na ndio kampuni yangu ikapata usajili.

Sasa mimi nadhani mswada huu ungekuja mapema na Mhe Rais akausaini ukawa sheria, basi mimi ningekuwa na makosa ya kutoa rushwa na nikapelekwa mahakamani. Maana yake naamini Mhe. Spika, kama mswada huu ungepitishwa na kuwa sheria, basi utapunguza rushwa kwa kiasi kikubwa sana.

Kwa hivyo, niendelee kumsifu Mhe. Waziri pia niwanasihi Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa juu sana tuupitishe mswada huu, ili haya mambo ya rushwa katika nchi yaondoke. Kwa maana hiyo, yule mwenye kusajiliwa awe na uwezo sio tu mtu anakwenda kukopa fedha anakwenda kwa mamlaka husika kutoa rushwa kumbe vile hana uwezo.
Mhe. Spika, nadhani mswada huu utatusaidia sana na pia niendelee kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe, kwamba mswada huu tuupitisheni na wala tusiukwaruze huu mswada kwa ajili ya kupata ufanisi katika nchi.

Jambo jengine Mhe. Spika, mimi nafikiria kwamba mswada huu katika madhumuni nilipoangalia taaluma ya hao wafanyabiashara zimetiliwa mkazo. Kwa hiyo, nawapongeza kwamba lazima tuangalie taaluma ya mtu kabla ya kumpa usajili, yaani kile anachokiombea au ile biashara anayoiombea usajili.

Kwa mfano, mtu anataka kuomba kuwa mchoraji, hivi kweli amesomea mambo haya au ikiwa anataka kuwa *contractor* na isijekuwa mwalimu kama mimi halafu unakwenda kuanzisha kampuni ya ujenzi, nadhani katika hili mswada pia umegusia mambo kama haya.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende katika sifa za Mkurugenzi Mtendaji kwenye ukurasa wa 107 ibara ya 6(2) (b), ambacho kinaeleza Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

Ukurasa wa 107 kifungu cha 6(2) (b) kinaeleza hivi:-

"Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

6(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala atakayeteuliwa na Rais, ambapo sifa zake zitakuwa kama zifuatazo:-

2(b) ana shahada ya Sheria na Uongozi au inayohusiana na hizo kutoka katika Chuo Kikuu kinachotambulika".

Mhe. Spika, hapo sasa, kwa sababu *degree* ya sheria huyu wakala hapa anashughulika na mambo ya wafanyabiashara, yaani anashughulika na kusajili mali na biashara. *(Makofi)*

Sasa ukisema *degree* ya sheria na utawala, *public administration* kwa hiyo ni vyema itajwe hasa awe na *degree* ya utawala wa biashara, *business administration* awe nayo huyu au hiyo ya sheria, lakini hili neno utawala tu liondolewe na iwe ni utawala wa biashara, na ikiwa hana *degree* ya sheria basi awe na *business administration*.

Vile vile kuhusu ibara ya 9 hapa inasema kwamba kutoa mamlaka, Mhe. Spika kwa idhini yako naomba uniruhusu kunukuu kidogo.

Kifungu cha 9 kinaeleza hivi:-

"Mkurugenzi Mtendaji kwa maandishi anaweza kumpa mamlaka afisa yeyote kutekeleza kazi zote au majukumu yoyote aliyopewa yeye kwa mujibu wa Sheria hii au kanuni yoyote iliyotungwa chini ya Sheria hii".

Mhe. Spika, hapa hatutaitendea haki mamlaka kumpa uwezo huu, kwamba yeye tumwambie kama anaondoka ampe mamlaka mtu yeyote tu pale atakayeona anafaa yeye, basi hatutaitendea haki.

Kwa kweli yeye tumempa uwezo huu Mkurugenzi mtendaji kwa kuwa ana sifa karibu miaka saba ya uzoefu, ana *degree* ya sheria au kama hana ya sheria anayo *degree* ya utawala wa biashara na leo aje achague shemegi yake, amwambie kwamba mimi nasafiri kipindi hichi lakini wewe shemegi yangu ndio nakupa uwezo wa kufanya hizi kazi zote ambazo ninazozifanya mimi hapa.

Kutokana na hali hii, Mhe. Spika mamlaka itakuwa hatuifanyii haki kwa ibara hii, huyu tumempa mamlaka haya kwa sababu ya sifa, uwezo pamoja na uzoefu, na leo yeye tumwambie hii sheria impe uwezo tu, kwamba wewe ukiondoka chagua yeyote umuweke hapa, hapana.

Kwa hivyo, mimi nadhani ni vyema kukaa na Mhe. Waziri anayehusika na haya mambo na kumueleza kwamba mimi nina safari ya kwenda masomoni, lakini hebu tutafute katika hawa watendaji hapa nani mwenye uwezo wa kuchukua hii nafasi na sio yeye tu ajiamulie, kwa sababu katika *democratic institutions* zozote mambo huwa *decentralized*.

Sasa nadhani Mhe. Waziri aangalie utaratibu kwamba a-*decentralized democracy* kwa ile ofisi kuweza kutoa kile chombo kwamba nyinyi teueni mtu na mimi nasafiri au yeye huyu Mkurugenzi mtendaji ashirikiane na Mhe. Waziri katika kufanya uteuzi wake. Lakini tukisema tunamuachia yeye basi tunaweza tuna-*create a sort of Monarchy* akamchukua mwanawe aliyemzaa au baba yake mdogo na kumwambia mimi naondoka na wewe kaa hapa au akamchukua baba yake mdogo na hii na iendi hivyo.

Kwa hivyo, nadhani hii ibara ya 9 huyu Mkurugenzi mtendaji katika kutoa mamlaka ashirikiane na Waziri husika wa wizara au a-*decentralized democracy* katika ofisi na watu wa ofisi waamue achukue nani. Mhe. Spika, nafikiri baadaye Mhe. Waziri atatafuta lugha ya kisheria, kwa sababu mimi ni mtu wa kusema maneno tu na wala sio mwanasheria isipokuwa ni mwanasiasa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kama tulivyosema kwamba mswada huu ni *melten copper*, yaani shaba moto haitiliki mkono. Kwa hivyo, kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa leo. Pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi na mimi angalau nitie mkono japo tumeambiwa hautiliki, hivyo naomba nitie kidogo kwenye masuala mawili matatu, ili tupate kuupitisha mswada huu.

Mhe. Spika, kwa kuanzia nataka niipongeze serikali kwa kuona kwamba ipo haja sasa ya kuanzisha taasisi ambayo itashughulikia *specifically* na mambo ambayo yanahusiana na usajili wa biashara na mali pekee.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa kuliona hili kwa maana ya kwamba kuanzishwa kwa taasisi hii kutawapatia urahisi wafanyabiashara ambao watasajili biashara pamoja na mali zao kwa urahisi kuliko ilivyokuwa mwanzo, kwamba taasisi hii moja inashughulikia mambo ya usajili wa biashara pia ikishughulikia usajili wa vizazi na vifo.

Mhe. Spika, naomba tena niipongeze serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuona kwamba ipo haja ya kuweka Naibu Mrajis kwa upande wa Pemba ambaye pia naye atashughulikia mambo haya ya usajili wa biashara pamoja na mali. Kwa kweli hii itawasaidia sana wafanyabiashara wa Pemba kuwaondoshea usumbufu wafanyabiashara hao wa kufuata huduma ya usajili Unguja, hivyo kuwapa usumbufu, lakini kuwapotezea muda wao ambao wangeutumia kufanya mambo yao ya kibiashara.

Mhe. Spika, pengine wapo ambao wanaotaka kusajili biashara zao, lakini wakifikiria kwamba mpaka waje Unguja kwa ajili ya kusajili na ukitizama vyombo vyetu vyenyewe ndio hivyo kila siku vinapinduka huwawia vigumu pengine kuja na kufanya usajili Unguja. Kwa hivyo, tuishukuru serikali kwamba imeliona hilo na hivi sasa wafanyabiashara watakuwa wanasajili biashara zao huko Pemba.

Vile vile katika suala hili la kuwawekea Naibu Mrajis dhamana Pemba, hivyo niipongeze serikali kwamba kutapelekea kuongezeka mapato yanayotokana na ada za usajili wa biashara na mali, kwa maana ya kwamba serikali imerahisisha huduma hii kupatikana Pemba na hivyo mapato mengi yatapatikana kutokana na huduma hiyo.

Mwisho Mhe. Spika, naomba niunge mkono hoja ya Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, ambayo alisema kwamba kwenye sehemu ya tatu uteuzi wa Mkurugenzi mtendaji kwamba sifa ambayo aliyokuwa anatakikana ya uzoefu ya Mkurugenzi huyu ni miaka saba. Kwa hivyo, mimi niunge mkono yale ambayo Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa amesema na niunge mkono kwa hoja ile ambayo kwamba kuna vijana wetu nje ambao hawana kazi na huu uzoefu wa kazi ni muda mkubwa.

Kwa kweli suala hili pia tuliliona kwenye Kamati na tulikubaliana kwamba miaka hii ipungue, sasa labda Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya maelezo atatupa maelezo kwamba imekuwaje.

Mhe. Spika, mwisho naunga mkono mswada huu na ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wajitokeze na kuujadili na mwisho tuupitishe mswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Spika, na mimi nashukuru mchana huu kunipatia fursa iliyo wazi ya kuzungumzia machache kuhusu mswada huu.

Mhe. Spika, nia ya serikali hivi sasa naona ni nzuri na kwa ujumla mswada huu umekuja wakati mzuri sana, tukiwa na malengo ya kuiweka nchi yetu katika hali nzuri.

Nikiangalia hapa madhumuni ya mswada huu moja ni kwamba kupunguza gharama za usajili pamoja na kuondoa misururu wakati wa usajili. Kwa kweli hii ni furaha kwa wananchi, basi ningependa kuona kwamba zoezi hili linafanyika kwa umakini mkubwa, ili lengo tulililokusudia lipatikane.

Mhe. Spika, katika sheria hii Mhe. Rais amepewa *option* ya kuona kwamba ikiwa kutakuwa na umuhimu wa kumchagua Naibu Mkurugenzi Mtendaji afanye hivyo, laa kama akiona hakuna basi aachie tu mambo yaende hivyo hivyo.

Kwa hivyo, mimi nafikiri tungesema tu moja kwa moja kwamba kwa hivi sasa na kwa kazi ambazo zitafanywa na sheria hii, basi Mkurugenzi mtendaji atakuwa anatosha hasa kwa vile na katika Kisiwa cha Pemba atakuwepo ambaye anamsaidia huyu Mkurugenzi mtendaji. Sasa ikiwa yeye atakuwa hayupo yule mkurugenzi mtendaji, basi yule wa Pemba anaweza tu kuja kuchukua nafasi mpaka huyu mwengine kama amekwenda masomoni au amekwenda likizo akachukua nafasi yake.

Mhe. Spika, mimi nimeona hakuna haja na itakuwa ni utumiaji wa fedha tu za wananchi wanaotoka jasho kila leo bure. Kwa maana hiyo, nafasi hii mimi ningesema tu moja kwa moja tukaiondoa na isiwepo katika sheria hii, kwamba Mkurugenzi mtendaji mmoja basi angetosha kufanya shughuli hizi. *(Makofi)*

Jambo jengine katika sheria hii Mhe. Spika tumeeleza jinsi gani tutampata Mkurugenzi mtendaji na tukasema kwamba awe na uzoefu usiopungua miaka saba. Mimi nadhani tusiende mbali sana miaka saba kwa nchi yetu na shughuli kama hizi ni mingi, labda tungeangalia uwezekano mwengine na kuipunguza hii miaka na tukaiweka kuanzia mitatu hadi mitano, lakini saba ni mingi mno.

Vile vile katika hilo, ili kumpata huyu Mkurugenzi basi tunaambiwa awe na shahada ya kwanza, hii sheria imani yangu kwamba itatumika kwa muda mrefu sana. Sasa ninachokiona hivi sasa katika nchi yetu ni kwamba vijana wengi wamejitokeza kuomba masomo hasa ya vyuo vikuu na kama tulivyoona mara hii kwamba Baraza hili limepitisha ongezeko la fedha ambazo zitatumika na wananchi kwa ajili ya mikopo. Kwa kweli hii yote tunawawezesha wanafunzi au vijana wetu kusoma katika shahada ya kwanza.

Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba baada ya miaka mitano inayokuja mbele shahada ya kwanza ya chuo kikuu labda nitaifananisha na *Form IV*. Mhe. Spika, mimi ninaona mtu ambaye tungempa kazi kama hii basi akawa na shahada ya pili ya chuo kikuu na sio shahada ya kwanza.

Mhe. Spika, jengine nililoliona kwenye sheria zetu ni kwamba mara nyingi tunakuwa tunatoa uwazi au upenyo. Kwa mfano, ukiangalia huku utakutia kwamba, ili kama mtu ametiwa katika hatia na ametenda kosa hakimu anapewa *option* kwamba aidha atoe faini kuanzia shilingi milioni 1,000,000/= au mpaka 3,000,000/=. Hii nafikiri ni fursa ya kumpa hakimu mwanya wa kutafuta chochote.

Sasa mimi ningependekeza kwamba sheria zetu zikawa *fixed* ikiwa mtu amebainika kwamba ametenda kosa la aina fulani, basi adhabu isiwe na *option* na wala isiwe hivi au vile na iende sehemu moja tu na iseme kwamba adhabu yake ni shilingi milioni 1,000,000/= au 2,000,000/=.

Kutokana na hali hii, nina wasi wasi hapa wakagawana kama ni shilingi milioni 3,000,000/= basi mshtaki na hakimu wakapata fursa ya kugawana, kwa sababu mimi ninao uwezo wa kuwambia shilingi milioni 3,000,000/= lakini bwana wewe nitakutoza shilingi milioni 1,000,000/= na shilingi milioni 1,000,000/= uniwekee mwenyewe tuje tuonane nyumbani. Mhe. Spika, kwa kuepuka hayo, basi ningependekeza hizi sheria zikaja katika mfumo kama huo.

Jengine Mhe. Spika kuna kinga kwa ajili ya Mkurugenzi mtendaji, yeye kwa sheria hii anayo kinga kwamba yeye hataweza kushtakiwa. Mhe. Spika, nafikiri katika nchi yetu mtu mmoja tu ndiye ambaye yuko *above the law*, sasa labda tuweke mazingira ambayo Mkurugenzi naye akifanya kosa basi atiwe katika hatia na wala tusiweke kwamba yeye asiweke katika hatia yoyote, kwa sababu huko tunakokwenda ni kwengine na wala tusimpe meno makubwa kiasi kama hichi.

Kwa kweli hali hii inasikitisha kwamba hata hawa maafisa wengine wadogo wadogo basi na wao wanayo kinga kama hii, mimi nafikiri sheria haikubali katika nchi zetu, hivyo nayo tungeifanyia marekebisho.

Mhe. Spika, hayo machache niseme naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuchangia mswada huu ambao uko *logical* kabisa, tena wenye kwenda na wakati muafaka kabisa. Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wa mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu.

Pia niishukuru Kamati kwa kutoa maoni, ambapo kamati hii ni *over site*, kwani Katiba na Sheria ni mambo mazito kama hatukuwa makini tunaweza kuleta athari kubwa. Kwa hivyo, naipongeza sana Kamati hii kwa jukumu kubwa hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, biashara ni jambo la muhimu na kwenye biashara ni lazima kuwe na mtaji wa kutosha. Kwa hiyo, ninawaomba wafanyabiashara sasa wajitokeze kujisajili na pia wawe na utayari wa kupata elimu ya mambo ya biashara, ili wafanyabiashara wawe na uhakika wa kile wanachokifanya.

Mhe. Spika, niwaombe wafanyabiashara wachukue mikopo katika Benki ya Watu wa Zanzibar pamoja na kuweka fedha zao kwenye benki hiyo, kwa ajili ya kuleta maendeleo ya benki yetu na kunyanyua uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa sababu hii taasisi ndio imeanzishwa kwa hiyo kutakuwa na mambo na itakapopitishwa sheria hii basi ningeiomba kwa sababu kuna kifungu hapa kinahusu mambo ya mapato, hivyo mapato ni kitu muhimu na mapato haya yatakuwa ni serikali.

Kwa maana hiyo, naomba kuwe na uadilifu zaidi kwani tumezoea katika taasisi nyingi za serikali hasa pale tunapokwenda Kamati yetu ya *PAC* tunakuta mapungufu ya uwekaji wa mahesabu ikiwemo *fixed asset register*, pia na mapungufu ya sheria ya manunuzi. Kwa hivyo, ninaomba sana ikipita sheria hii basi zile sheria nyengine zote za manunuzi ziwe zinafuatwa.

Mhe. Spika, nishukuru sana mwezi uliopita tulihudhuria semina ilikuwa ni Mkutano wa 9 wa *SADCOPAC*, ambao ulikuwa na dhana ambayo iliyosema "*improving the effectiveness of Public Accounts Committee to whole the government to account for the use of public sector resources"*. Kwa hivyo, ni kukuza ufanisi wa Kamati za *PAC*, kuikamata serikali kuwasilisha matumizi ya *resources* za umma.

Mhe. Spika, mimi kama Mjumbe na Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, niseme baada ya kupita sheria hii basi ni lazima zile sheria za fedha na manunuzi zizingatiwe.

Kwa kweli Mhe. Spika sheria hii ni nzuri na vifungu vyote kama ilivyotangulia kamati husika, basi na mimi niseme kwamba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Amani naunga mkono sheria hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai na kuweza kukutana hapa hivi sasa. Vile vile nichukue nafasi kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kusema machache katika mswada huu.

Pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa umahiri mkubwa ambao wameweza kuufanya mswada huu

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaokwenda kupumzika nje tunakusudia mswada huu umalizike kipindi hichi cha asubuhi kabla ya jioni, kwa sababu tuipate hii *quorum* na kuitumia.

Kwa hivyo, nina wasi wasi mkubwa kwamba *quorum* hii ikawa ngumu kutokana na mashughuli mengi ambayo yametukabili. Kwa maana hiyo, tuitumie *quorum* hii kwa ajili ya kumaliza shughuli hii na ninao wachangiaji wawili tu waliobakia.

Mhe. Panya Ali Abdalla, endelea.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante niendelee kutoa pongezi kwa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake ambao wameweza kutuletea mswada huu kwa wakati muafaka ambao utaweza kutusaidia.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika kifungu 8(1) (b) na kwa ruhusa yako naomba kunukuu kifungu hicho.

Kifungu cha 8(1) (b) kinaeleza hivi:-

> "Kukataa kuifanyia usajili nyaraka yoyote, hati ya usajili au nyaraka nyengine ambayo maelezo yake yatahitajika kutolewa au kuzuiliwa kutolewa au iwapo kitendo chengine chochote kitatakiwa kutekelezwa chini ya Sheria hii au kutotekelezwa kwa Sheria yoyote inayohusika; kwa kufanya hivyo Mkurugenzi Mtendaji atatakiwa kutoa sababu ya kukataa kwake".

Mhe. Spika, kwa kuwa Mkurugenzi mtendaji ni binadamu kama walivyo binadamu wenzake atakuwa na yeye anayo mapungufu kama waliyonayo binadamu wenzake. Kwa kuona Mkurugenzi mtendaji asije akawa pengine ana chuki binafsi ya mtu ambaye anataka kumsajili.

Ushauri wangu namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aweze kuunda bodi hapa ambayo itaweza kumshauri Mkurugenzi mtendaji katika kuchuja majina ya usajili ya wenye sifa za kusajiliwa. Kwa kweli hii itaweza kumsaidia Mkurugenzi na kumfanya Mkurugenzi mtendaji aondokane na kutoa sababu za kukataa kwake.

Jambo jengine Mhe. Spika, kama tunavyoelewa sheria nyingi ambazo tumezitunga na zimeshapitishwa. Lakini kuna tatizo ambalo zinazifanya sheria zetu kutotekelezeka kiurahisi. Mhe. Spika, sheria huwa zinachelewa sana kutumika kwa ajili ya ucheleweshwaji wa utungwaji wa kanuni.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba itakapopitishwa sheria yake hii basi aharakishe katika utungaji wa kanuni, ili iweze kuwasaidia wafanyabiashara haraka iwezekanavyo, kwa sababu kama tunavyoelewa kwamba mtu huchonga mwiko kwa kunusuru mkono kuungua.

Mhe. Spika, sheria hii itakapokuwa tayari basi itaweza kuwasaidia wafanyabiashara wetu, waweze kufanya biashara zao hali ya kuwa wanatambulikana.

Mhe. Spika, jengine katika kifungu cha 7 pamoja na utendaji wa kazi wa Mkurugenzi mtendaji, basi mimi ninaomba pia mkurugenzi mtendaji huyu akaandaa mpango kazi ambao ungeweza kumsaidia yeye katika majukumu yake ya utendaji wake. Pia mpango kazi huu ungeweza kumsaidia waziri katika kutoa ripoti zake kila baada ya miezi mitatu.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mswada huu umejengeka katika sura nzuri na mimi nimeanza kutanguliza pongezi mwanzo nasema Mswada huu nauunga mkono kwa asilimia mia moja. Naomba na wenzangu wauchangie na baadae tuunge mkono kwa pamoja ili wafanyabiashara wetu waweze kusajiliwa vizuri.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kuniruhusu dakika tano kuuchangia Mswada huu muhimu. Nije ukurasa 106 bila ya kupoteza wakati juu kifungu kinachosema uanzishaji, wakala na usajili wa biashara na mali Zanzibar.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya Kampuni ambazo hazina uwezo zinaendesha biashara zake bila ya kuangalia maslahi ya nchi pamoja na wananchi wake. Kuna kampuni nyengine zina uwezo kwa Mswada huu utaupa uwezo kufanya kazi kwa usanifu kabisa. Kuna baadhi ya kampuni nyengine tumeziona uwezo wake ni mdogo na cha kusikitisha zaidi kuna kampuni za wazawa hapa huwa hazipati nafasi na huja zikapewa kampuni za kigeni. Tumeshuhudia uwezo wake baadhi ya kampuni hasa katika kampuni za ujenzi. Tumeshuhudia baadhi ya kampuni zikawa zinajenga hapa zikawa zinatia vitu ambavyo vinalingana na *standard* yake, tofauti na kampuni ziliopo hapa za Wazanzibari wazawa.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije Sehemu ya Tatu ya Uongozi na Wakala, kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala akiteuliwa na Rais. Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa na kuwa Mkurugenzi Mtendaji iwapo ni Mzanzibari. Hapa mimi nataka nipasifu sana kwa nafasi kwamba atapewa Mzanzibari mwenye uwezo.

Mhe. Spika, kwa kweli huu Mswada hautaki kuchangiwa sana, umejitosheleza kabisa. Hii inatokana na Mhe. Abubakar kutokana na uwezo wake na sifa zake jinsi anavyojipanga kuwa hapati vizingiti humu ndani kutokana na uzowefu wake alio nao. Baada ya hayo machache, Mheshimiwa naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii nikaweza kuzungumza machache katika Mswada huu wa Uanzishwaji wa Sheria ya Uwakala wa Biashara.

Mhe. Spika, mimi kwa mara nyengine tena nataka niipongeze sana serikali yetu kwa kuwa sasa hivi katika kila Mswada unaoanza kuja unatuonesha kwamba serikali yetu inaanza kuangalia uono wa mbali, hatuangalii tu ya hapa hapa, lakini tunaangalia kuimarisha maisha ya wananchi.

Mhe. Spika, Mswada huu ukiuangalia kijuu juu naona kama unaanzisha hii Sheria ya kuweka uwakala wa usajili wa biashara. Lakini ukiuchambua kwa undani Mswada huu Mhe. Spika, huu ndio unatekeleza hasa yale malengo ya Mileniam yaani pamoja na Mkuza.

Mhe. Spika, kijumla jumla Mswada huu unazungumzia zaidi usajili wa Makampuni, biashara mbali mbali, NGOs mbali mbali. Haya yote yanakuja kwamba lengo lake ni kuinua mapato ya serikali. Kuinua mapato ya serikali, moja ni kuweza kuwa na takwimu sahihi. Unapokuwa na takwimu sahihi ya makampuni mangapi yapo, wafanyabiashara wangapi wapo na wanafanya nini kwa mtaji wa aina gani, kwa hiyo utairahisishia serikali kupitia bodi ya mapato Zanzibar kuweza kupanga vizuri malengo yake katika ukushanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, Mswada huu kwa kweli itakuwa ni kielelezo kikubwa kwa Mhe. Waziri wa Fedha pale anapokuja kuanza kuangalia mapato ya nchi, lakini vile vile na malengo na matarajio ya serikali. Wananchi wetu huko nje mara nyingi wanajiuliza tunapopitisha hii Miswada wao wanafaidika nini. Nadhani Mswada huu unalenga mpaka kuongeza ajira katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nataka nitoe ushauri. Sasa hivi katika Mswada huu umeangalia zile biashara tunazoweza tukasema zile zilizokuwa rasmi. Mimi mapendekezo yangu kuzishauri Halmashauri kujaribu kuangalia na zile biashara zisizokuwa sio rasmi basi nazo pia ziweze kuwa na usajili, si lazima usajili wake upitie kwa huyu msajili wa makampuni lakini angalau katika zile Halmashauri au Manispaa ili kuweza kujua ni nani na nani anaefanya biashara.

Mhe. Spika, hii itaweza kuja kusaidia mpaka kwa zile taasisi ambazo huwa zinatoa mikopo midogo midogo au zinatoa misaada ya aina mbali mbali au hata kutoa taaluma mbali mbali kwa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo wa vijijini na hata mjini wapo wafanyabiashara wadogo wadogo. Hili haliishia hapo, hili litaweza kusaidia hata zile Benki ambazo zimeanzisha ile mikopo kwa ajili ya kuhamasisha hizi sakos kuweza kujua hawa wafanyabiashara wadogo wadogo katika Shehia fulani au katika eneo fulani wapo wangapi, ili kuweza kujua mabenki haya au taasisi za kifedha zikiingiza fedha zao kule zitaweza kuwasaidia wananchi wengi na kuweza kuwaondolea umasikini.

Mhe. Spika, Mswada huu kwa kuwa ni mtambuka, mimi nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wa Biashara pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha. Hapa Zanzibar wafanyabiashara wetu wengi sana hasa wadogo wadogo mpaka wakubwa wanaupungufu mkubwa ya kufanya biashara. Taaluma ya kufanya biashara sio kujua kufanya ile biashara peke yake, lakini mbinu za kuweza kutanua mbinu za biashara zao. Vile vile mbinu za kuweza kutafuta mitaji, nitatoa mfano.

Mhe. Spika, hivi sasa hivi tumejaribu kuangalia wenzetu Tanzania Bara kuna baadhi ya hizi benki huwa wanajaribu kutoa semina kwa wafanyabiashara wao wadogo wadogo kwa wale wateja wao kujaribu kuwafahamisha namna ya kuweka hakiba, namna ya kuongeza mtaji, lakini vile vile kuweza kuifanya ile biashara isiyokuwa rasmi iwe rasmi ili iweze kutambulika mpaka kwenye vyombo vya fedha kwa ajili ya kuweza kuongezewa nguvu.

Mhe. Spika, sasa hivi hapa Zanzibar kuna baadhi ya wafanyabiashara au kuna baadhi ya kampuni wakati mwengine wanakuwa na kazi kubwa, lakini uwezo wa kuweza kumudu kuifanya ile kazi inakuwa ni mdogo hasa katika suala zima la kipato. Lakini hapa kama ingelikuwa wana taaluma ya kutosha wangelikuwa hizi taasisi za fedha zinatoa taaluma ya kutosha, nadhani makampuni haya yangelikuwa na uwezo mkubwa kuweza kufanya kazi.

Mfano ukiangalia hii sera ambayo serikali yetu imeianzisha ya *Public Private Partnership* (PPP) katika eneo muhimu sana katika biashara katika nchi yoyote duniani ni eneo hili. Lakini bado kwa upande wetu Zanzibar wafanyabiashara wengi hili hawajalianzisha. Biashara ina mambo mengi, kuna wengine wana utaalamu wa biashara lakini wana upungufu wa mtaji. Kuna wengi wana fedha nyingi lakini hawana utaalamu wa biashara. Sasa kama wanaanzisha PPP si lazima iwe inashirikiana kwa *government* moja kwa moja. Hata kwa wafanyabiashara wenyewe kufanya ile *share holding* hii wanaweza kufanya biashara kubwa na ikaleta tija kubwa katika nchi.

Mhe. Spika, hapa leo tunalalamika kuna baadhi ya kazi wanapewa makampuni pengine kutoka nje ya Zanzibar. Wakati mwengine hii inatokana kwamba makampuni yetu wakati mwengine mitaji yao midogo, uzoefu wa kazi unakuwa mdogo na maarifa na wataalamu wanakuwa wachache. Sasa kama wafanyabiashara wanapata taaluma wanaweza kuunganishwa kwa kushirikiana kwa kuunganisha fikra zao tofauti tofauti, wale wenye maarifa wenye mitaji na wenye maeneo.

Mhe. Spika, kuna watu wengine wana mtaji, wanataka kufanya biashara lakini eneo hana. Kuna watu wengine hasa Zanzibar, watu wengi wana ardhi nyingi tena ardhi kubwa lakini hazizalishi. Lakini kuna watu wana fedha lakini

hawana ardhi za kuweza kufanyia kazi. Taaluma hii mimi nafikiri Mhe. Waziri wa Biashara kama ataweza kuelimisha vijijini, mimi nadhani wananchi wanaweza wakatangaza ardhi zao.

Mfano wenzetu sasa hivi Bara wameanzisha kupitia *TBC* huwa naona matangazo ya biashara wanatoa matangazo ya kuuza nyumba, kuuza magari, kuuza viwanja, kuuza maeneo. Sasa mimi nadhani na hapa kwetu Wizara ya Biashara ingejaribu kuhamasisha jambo hili kwa wale wananchi ambao wana *plot* ambao hawana fedha hawajui *plot* zile wazitumie kwa ajili ya biashara gani. Mimi nafikiri mtu angelisema mimi nipo Paje, nina eneo langu pengine lina ekari 20 liko zuri, lipo karibu na ufukwe, kama kuna mtu ana fedha zake aje kuwekeza tuingie ubia. Taaluma hii kwa hapa Zanzibar hatuna.

Mfano mdogo kuna watu ambao wanatumia maarifa yao tu, mtu hana ardhi lakini anajua kuna watu wanatafuta ardhi na kwa kuwa yeye anaujua umuhimu wa ardhi anatoka anakwenda vijijini anainunua ardhi kwa bei ndogo baada ya miezi mitatu au miezi mine anamtafuta mtu mwenye fedha zake anakwenda kuiuza kwa bei ya mara kumi zaidi ya ile waliyoiuza wale wana kijiji. Utakuta kwa Zanzibar taaluma hii bado hatuna. Mimi nadhani kwa sababu leo tutasajili hapa makampuni zaidi ya mangapi, lakini mwisho wa mwaka unakuja kuuliza makampuni haya je mtaji wao wameweza kuzalisha kiasi gani. Unaweza ukakuta tuna orodha nyingi Makampuni lakini tija ndogo na kilichofanyika hakitambulikani.

Mhe. Spika, mimi nadhani sasa hivi ili wananchi waweze kujua sheria tunazozipitisha hapa zina umuhimu gani kwa maisha yao katika *program* ya kuondoa umasikini. Nadhani wakati sasa hivi umefika ili kujua kwamba sasa hivi tunajaribu kuwashajihisha wananchi wetu. Tulianzisha sheria nzuri hapa ya kurasimisha rasilimali ya mwananchi, yaani kama kuna mtu ana ardhi yake aweze kuikopea au ana *asset* yake aweze kuikopea. Lakini je, tokea tulipopitisha sheria ile kuna wananchi wangapi ambao wamefaidika na sheria ile. Kwa sababu hawajui kitu, sisi tunapitisha hapa tukisha kupitisha wananchi hata hawajui kwamba sheria ile inawapa miongozo ya kiasi gani.

Mhe. Spika, mimi nadhani kwa wale watu wa maeneo ya vijijini hasa maeneo ya ukanda wa pwani sasa hivi hebu wangelijaribu kutumia hii taaluma. Mimi si mtaalamu wa biashara lakini huwa najaribu kuangalia wenzetu nini wanachokifanya na wanaweza kufaidika kiasi gani.

Mhe. Spika, kuna wananchi sasa hivi wanajenga majumba yao na wakati mwengine wanachukua mkopo Benki, yeye anayo nyumba lakini amejenga nyumba nyengine. Lakini jumba lile linakaa linafika pahala mpaka linaota mwitu, wakatu huku kuna watu wanatafuta nyumba za kukodi lakini hawajui nyumba watazipata wapi. Mimi nadhani tuanzishe utaratibu wa kutoa matangazo ili itaweza kuwasaidia wananchi zile asset zao ziweza kuwasaidia wao wenyewe.

Mhe. Spika, mimi katika mtu mmojia ambaye nilikuwa siku zote nilikuwa nailalamikia BOT. Kwa sababu wenzetu kule Bara wanatoa mikopo mpaka inafika bilioni 4 kwa ajili ya (*small and medium enterpris*) yaani kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wakati. Lakini Zanzibar hapa mpaka hii leo ninavyozungumza bado wafanyabiashara wa Zanzibar hawajaitumia fursa hiyo. Kwa nini hawajaitumia fursa hiyo, hawaitaki? Kwa sababu hawanja taaluma nayo.

Ndio maana nikasema Mswada huu ni mtambuka kwa sababu ni Mswada, utaona ni wa kusajili tu lakini huu ni Mswada wa kitaalumu wa kiuchumi. Mimi nadhani Mhe. Waziri wa Fedha angalijaribu sasa kuzungumza na BOT, wakaandaa warsha moja kubwa, wakawaita wafanyabiashara wa kati pamoja na wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuweza kuangalia ni maeneo gani wanaweza wakashirikiana ili wakaweza kuitumia hii fursa iliyokuwepo BOT kwa ajili ya kutumia fedha hizi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu. Wakiweza kutoa semina hiyo, wakiweza kutoa utaalamu huo hawa wataweza kuinua mitaji yao, wataweza kuanzisha biashara mpya ya wataweza kutoa ajira.

Mhe. Spika, najua unataka kunambia nimalizie malizie lakini mwisho kabisa kabisa nataka niseme kwamba naishukuru sana serikali kwa kusema kwamba mfumo huu ulioanzishwa sasa hivi utaweza kupunguza mpaka ile gharama ya usajili. Vile vile itaanzisha mfumo wa kuweza kutambulikana makampuni ya Zanzibar kutambulika kimataifa.

Mhe. Spika, sijui mpaka sasa hivi kama kuna kampuni hapa Zanzibar ambayo iliyokuwa inajulikana kazi zake kimataifa na uwezo wake uko vipi ili makampuni mengine au wafanyabiashara wengine waweze kuvutiwa kuweza kufanya *join venture* na makampuni yetu ya Zanzibar. Naamini kupitia sheria hii ikiwa tutaifanyia kazi vizuri, ikiwa

biashara zote zimo katika mtandao, mimi nadhani watu wengi wataweza kuvutiwa ili kuweza kuja kufanya biashara hiyo.

Mwisho kabisa kabisa Mhe. Spika, kuna kampuni ambayo wanataka kujenga nyumba hapa Zanzibar, hii kampuni ipo tayari, wameshajisajili, wameshakwenda mpaka China, tayari wameshapata Kampuni ya kuweza kuwaingizia fedha karibu dola milioni 500 kwa ajili ya kujenga nyumba hapa Zanzibar. Lakini je, tuulize fedha hizo wakishakuzipata riba yake ipo ndogo, eneo la kujenga nyumba watalipata wapi. Hawa wanataka kutengeneza mji, wamenambia wanataka kulichukua eneo lote lile la Makadara wajenge nyumba za gorofa tano tano, ili wananchi wahame kwa muda baadae warudi pale na wenyewe sasa hivi wananisikia na ndio napiga debe hapa. Maeneo mengine yatakuwa ni yao wenyewe ile kampuni.

Je, serikali iko tayari kushirikiana na hawa, kwa sababu wapo ndio maana tukasema Mhe. Spika, sasa hivi Wazanzibari wameshajanjaruka, tayari wameshashirikiana na kampuni mbali mbali duniani, fedha zipo na hivi juzi tulivyokwenda Zambia Mhe. Spika, wewe ulikuwa shahidi, mimi, Mhe. Makame Mshimba na Mhe. Omar Ali Shehe, kuna kampuni sasa hivi wako tayari kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kujenga ule Uwanja wa Watoto, kujenga majengo ya aina yoyote wanayotaka kwa mkopo wa riba nafuu. *ZSSF* mpaka leo wanaingia huku, wanatoka huku, fedha zipo watu fedha wanazo mnaogopa kuchukua pesa.

Mhe. Spika, makampuni haya hawataki pesa ya serikali wao wanataka kuingiza pesa yao serikali i-*guarantee* tu. Hizo fedha wako tayari wataziingiza ndani ya Benki ya Watu wa Zanzibar ili yale makapuni yatakuwa yanachukua fedha zile. Kwa hivyo serikali ikitoa *security* fedha zile zitakuwa zipo ndani ya mikono ya serikali, zimo ndani ya benki ya serikali.

Mimi najiuliza tunapitisha sheria hizi zote watu wanakuja na fedha tunawapiga chenga mpaka leo, tunasubiri ninini. Mhe. Spika, naomba Mawaziri mimi nimezungumza haya kama wanahitaji maelezo ya ziada mimi nitakaa nao nitawaletea hao wawekezaji ili waweze kusaidia uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, la mwisho sitaki kulisema kwa sababu hilo liko chini ya Ofisi yako, najua linakwenda vizuri PPP inakwenda vizuri. Naamini kuna jambo zuri ambalo litaweza kuleta maslahi kwa Zanzibar na kwa Wazanzibari baada ya muda mchache tutakaa sisi na serikali tumeshazungumza na Makamo wa Pili wa Rais naamini nilikifanikiwa hilo basi huu Mswada wa Sheria utakuwa ni mzuri. Huu ndio unakuja kuleta hiyo njia na muongozo ya kuweza kutuondoa hapa ili tuende huko tuliko.

Mheshimiwa tuchangamkie fursa za ndani kwanza halafu baadae tuzungumzie zilizokuwa za Muungano na sehemu nyengine. Bado Zanzibar tunavyo vipaji, tuna watu wana maarifa mazuri ya kuweza kuendeleza maisha ya watu wa Zanzibar kama tutashirikiana vizuri.

Jengine nitakuja kulimalizia kesho nitakapokuja kuwasilisha Mswada wangu wa marekebisho ya Sheria ya Vitambulisho vya Uzanzibari, kuna jambo jengine muhimu sana nitakuja kulieleza ili kwa manufaa ya Wazanzibari wote na Tanzania kwa jumla.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nakushukuru na naunga mkono hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo kuhusu mambo ambayo yamekuwa *raised* katika Mswada wangu huu.

Mhe. Spika, kwanza napenda nitoe shukurani za dhati kwa Kamati ya Katiba na Sheria kamka kawaida Kamati hii imekuwa na msaada mkubwa sana kwa wizara yangu. Mimi napenda nichukue nafasi hii kuishukuru tena kwa kushirikiana kwao na sisi ili kwa kusukuma mbele shughuli zetu hizi za kitaifa.

Mhe. Spika, marekebisho ambayo yamezungumzwa na Kamati ya Katiba na Sheria yote tunakubaliana nayo na yale aliyoyasema Mhe. Ali Abdalla naomba ichukuliwe katika *Hansard* kwamba yale ni marekebisho ambayo tumekubaliana.

Ningelipenda niseme kwamba katika marekebisho yale maelezo mengi ambayo yametolewa na baadhi ya Wawakilishi yamo majibu yake katika marekebisho yale. Kwa mfano Kamati ya Katiba na Sheria ilizungumzia kuhusu Mkurugenzi Mtendaji kwamba mbali na sifa alizonazo lakini miaka saba walisema kwamba ni mingi sana na wao walirekebisha wakasema badala ya miaka saba iwe miaka mitano. Wajumbe katika kuchangia kwao katika kifungu cha 6 ile kusema kwamba "ana uzoefu wa miaka saba" ile imeshafutwa. Kama alivyosema kwamba tumekubaliana na Kamati ya Katiba ya Sheria badala ya miaka saba iwe ni miaka mitano.

Mhe. Spika, hivyo hivyo kwa Naibu Mkurugenzi Mtendaji, badala ya miaka mitano tumekubaliana iwe miaka mitatu. Lakini katika hilo Mhe. Spika, naomba niseme kwamba katika kifungu cha 6 pale kuna sifa za nani anaweza kuwa Mkurugenzi Mtendaji, kwanza ni lazima awe ni Mzanzibari. Napenda kuchukua nafasi hii kujibu kwamba hapa tunachokusudia ni kwamba awe ni Mzanzibari wa ukweli. Najua kama alivyosema Mhe. Hija Hassan Hija kwamba kuna matatizo ya kufoji baadhi ya vyeti.

Napenda nimuhakikishie kwamba si hapa tu, lakini wakati wowote tunapoviona vyeti ambavyo vimekuwa vya kufoji tumeshavi-*cancel* vyeti vingi. Hivi karibuni tuli–*cancel* chetu cha mtu ambaye anatoka Congo na baada ya kujua tukachukua hatua na watu wengine ambao wanafoji vyeti kama hivyo. Kwa hivyo asiwe na wasi wasi tunapozungumzia suala la Mzanzibari tunakusudia Mzanzibari wa kikweli kweli na sio wale wanaofoji.
La pili lilizungumzwa sana kuhusu Shahada ya Sheria au uongozi au inayohusiana na mambo hayo na wengine wakasema kwamba kuwe na mtu au Shahada nyengine au uzoefu mwengine uwe ni suala la biashara.

Kwanza napenda niseme kwamba Sheria hii madhumuni hasa ni suala la usajili. Kama mtakavyokubaliana na mimi kwamba katika suala la usajili mambo mengi yanayohusiana na mambo ya sheria. Ndio maana katika hizi sheria saba ambazo tulizizungumza, tulisema kwamba sheria hizi ndizo ambazo huyu Mkurugenzi Mtendaji pamoja na wenzake watahusika nazo. Kwa hivyo *actually* hapa ukipata mtu mwenye uzoefu wa sheria basi ni aula zaidi. Lakini suala la biashara nafikiri hilo limechukuliwa maanani au limezingatiwa katika kifungu cha 6(2) (a) (b) na (c).

Kifungu cha 6(2) (C) "awe nja uwezofu wa kazi katika eneo hilo lisilopungua miaka mitano"

Sasa ule uzoefu ndio unamfanya na yeye aweze ku–*qualify* katika suala hili. Kwa hiyo anaweza akawe na sheria au shahada ya shughuli nyengine kwa mfano ya uongozi lakini kama anaouzoefu wa shughuli zile za biashara basi pia anaweza kuwa *qualified* kuingia katika msururu huu.

Mhe. Spika, katika hili pia lilizungumzwa suala zima la usajili huu au Mzanzibari huyu ambaye anataka kuteuliwa kuwa ni Mkurugenzi Mtendaji, wengine wakasema kwamba hakuna haja ya kuwa na msaidizi wake. Mimi nafikiri kile kifungu ambacho kinaelezea suala la kuwa na msaidizi ni kifungu ambacho kimewekwa hakizidishi wala hakipunguzi. Kinawekwa hapo kwa makusudi kwamba pale ambapo imetokea haja na shughuli pengine zimezidi. Kwa wakati huu kweli tunaweza tukasema kwamba hakuna haja, lakini hatujui mtiririko wa biashara na mtiririko wa shughuli ambazo zitakwenda. Inaweza ikatokezea haja, sasa wakati tukikifuta hichi kifungu tutapata matatizo itabidi lazima tuje tena katika Baraza ili tuweze kuomba mabadiliko *our amendment* ya sheria hii. Mimi nahisi kifungu kile kwa sababu hakizidishi wala hakipunguzi ni vyema tukakiwacha kama kilivyo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa ujumla naomba kwanza nije kwa Mhe. Ali Abdalla ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, kama alivyosema namshukuru sana kwa maoni yao na kwamba maoni yao tunayachukua kama ni masahihisho ambayo tumekubaliana nayo.

Mhe. Mshimba naye ninamshukuru kwa ushauri wake ambao ametupa na yeye ndiye aliyesema kwamba lazima kuwe na uzoefu wa biashara, nakubaliana naye kwamba katika hilo ni zuri, lakini kama nilivyosema katika kifungu cha 6, 2 (c) yale maelezo yake yote ambayo alipendekeza natumai yamezingatiwa katika cha (c) kwenye kifungu cha 6, 2.

Mhe. Omar Ali Shehe alizungumzia kuhusu kifungu cha 10 ambacho alisema kuhusu Naibu Mkurugenzi na akasema kwamba katika kifungu cha kumi Rais anaweza kumteua Naibu Mkurugenzi Mtendaji kama ataona ipo haja ya kumsaidia Mkurugenzi Mtendaji. Na mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa Naibu Mkurugenzi hapa badala ya miaka 5 tumesema au tumekubaliana na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba iwe miaka 3. Na suala jengine ni lile uzoefu wa biashara kama nilivyosema kwamba kifungu cha 6, 2 (c) nacho kinazungumzia hilo suala la biashara.

Mhe. Hija ninafikiri nimeshamjibu ni kwamba yeye ana wasiwasi kwamba huyu mzanzibari kweli atakuwa ni mzanzibari? Kama nilivyomwambia kwamba hawa watakuwa ni wazanzibari, lakini kama kuna mtu ataghushi au atabadilisha cheti hiki na baadae tukamjua kwanza kwa mujibu wa utaratibu wa sheria ni kwamba ameshaji-*disqualify* yeye mwenyewe. Kwa hivyo mtu kama huyo tukimgundua au kama kuna taarifa yoyote ambayo tutapata basi bila shaka atakuwa ameshaji-*disqualify* na uteuzi wake ule utakuwa si wa halali.

Mhe. Spika, Mhe. Mahmoud yeye pia alizungumzia kifungu cha 6 (c) na pale napenda niseme tu kwamba si miaka 7 kama alivyosema lakini kwa makubaliano na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ni miaka 5 kwa Mkurugenzi Mtendaji, na Msaidizi wake itakuwa miaka 3. Na hii Mhe. Spika, pia Mhe. Mahmoud alizungumzia kuhusu uzoefu, akasema kwamba kuna vijana wengi ambao wameshamaliza skuli, na vyuo na sasa tukiweka huu uzoefu tunaweza tukawapunguzia hawa.

Lakini naomba niseme mambo mawili katika suala hili, kwanza hapa ni mtu mmoja tu tunayemtaka Mkurugenzi Mtendaji si nafasi nyengine. Na Mkurugenzi Mtendaji ni kiongozi wa ile *institution* yenyewe kwa lazima uzoefu uchukuliwe. Sasa kwa watu wengine hatuna matatizo ni sawa sawa katika maeneo yote yale hata dereva wa gari kwa mfano kama utachukua gari la tani 30 ukamtafuta dereva lazima upate dereva ambaye ana uzoefu wa kuendesha magari yale angalau kwa miaka fulani, kwa sababu ni kitu ambacho atakuwa na dhamana nacho. Kwa hivyo hii Mhe. Mahmoud naona isikupe wasiwasi ni kwa sababu ya nafasi ya mtu mmoja, lakini nafasi nyengine anaweza aka-*apply* mtu yeyote kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa katika kanuni zetu au sheria zetu za utumishi.

Mhe. Subeit naye alizungumzia suala zima la usimamizi, mimi napenda nimhakikishie kwamba tutasimamia tukijaaliwa tukishirikiana pamoja na wao, na madhumuni hasa ukisoma katika kifungu cha 7 tumesema kwamba madhumuni ya sheria hasa ukisoma kifungu cha 7, 1(b) (d) na (g) inasema kwamba madhumuni tunataka kuweka kumbukumbu za usajili takwimu na kukusanya na kuwajibika na mipango yote kwa mujibu wa sheria zinazohusika. Kwa hivyo haya ndio madhumuni ya kutaka kujua zile sheria zinashughulikiwa vipi, kuweka kumbukumbu muhimu, kwa sababu zamani kama tunavyojua ni kwamba kila mtu alikuwa anasajili pake, hakuna kumbukumbu tunazoweza kuzipata kwa pamoja kama ni serikali. Kwa hivyo kitendo hiki cha kuwa na wakala wa usajili ina maana kwamba usajili wote utafanywa kwa pamoja, kumbukumbu zote zitapatikana kwa pamoja na hiyo itakuwa ni taarifa muhimu na taarifa nzuri kwa serikali.

Mhe. Saleh alizungumza sana kuhusu rushwa, mimi ninamuhakikishia kwamba tutajitahidi kuondoa rushwa na kama tunavyojitahidi lakini alisema kwamba kusajili hawa yule mtu ambaye anatakiwa *at least* awe ni kiongozi katika *department* hii awe ana business *administration* kuliko public *administration.* Kama nilivyosema hapa sisi tunazungumzia sana mambo ya usajili, na unaposoma *public administration* na unaposoma *business administration* najua kuna somo moja la sheria lazima ulisome. Sasa hiyo inaweza ikasaidia lakini pia uzoefu ndio tuliochukulia hapa. Mbali na kuwa ama awe na *degree* ya sheria au ya *public administration* kifungu cha (c) awe na uzoefu wa shughuli nyengine yoyote. Kwa hivyo nafikiri hii inaweza ikasaidia katika wasiwasi wake Mhe. Mjumbe kusema kwamba tunataka mtu ambaye ana sifa na uzoefu wa shughuli hizi. Ninaamini katika kifungu hiki kimeweza kusaidia kwa misingi hiyo.

Mhe. Spika, kifungu cha 9 ambacho kimezungumzwa sana ni kwamba Mkurugenzi anaweza akatoa nafasi akampa mtu yoyote yule katika kuendesha shughuli zake. Mimi ninafikiri huu ni utaratibu wa kawaida pale ambapo mdhamini wa sehemu fulani hayupo, kwa hivyo anawajibika wakati anaondoka kumpa mtu ambaye anahisi anafaa kumfanyia shughuli zake mpaka pale ambapo atarejea. Kwa hivyo kifungu hiki kinachofanya ni kutoa uhuru wa kisheria kwamba anaweza akamteua mtu ambaye anahisi kwamba anafaa katika utendaji wa shughuli zake katika kipindi kile ambacho yeye hayupo mpaka pale ambapo atarejea.

Mhe. Spika, Mhe. Wanu naye alizungumzia kifungu cha 6 na kifungu cha 6 kama nilivyokielezea kwamba kimerekebishwa badala ya miaka 7 sasa itakuwa miaka 5. Mhe. Abdalla Mohammed yeye alizungumzia sana kifungu cha 10 na akasema kwamba hakuna haja ya kuwepo uteuzi wa Naibu Mkurugenzi. Kama nilivyosema Mhe. Spika, ni kwamba haja tunahisi ipo kwa sababu shughuli hizi zinaongezeka mara kwa mara. Sasa shughuli zinapoongezeka na hapo ambapo tutahisi kwamba kuna haja ya kuteua Naibu Mkurugenzi kwa hivyo kifungu hiki kitatupa nafasi nzuri ya kufanya hivyo. Vyenginevyo tukikifuta hivi sasa haja zikaongezeka tukataka kuja kuteua Naibu Mkurugenzi kwa kweli tutakuwa tumejikwamisha na itakuwa si vizuri. Na zaidi akazungumzia kifungu cha 6

ambacho kifungu cha 6 nimeshakizungumza kwamba ni miaka 5 badala ya miaka 7 na Msaidizi wake atakuwa miaka 3 badala ya miaka 5.

Mhe. Spika, pia lilizungumziwa suala la adhabu kwamba iseme tu ni kiasi fulani. Mimi napenda niseme tu utaratibu wa kisheria huwezi tu kusema tu kwamba adhabu kwa kosa hili itakuwa shilingi milioni moja. Kuna makosa maalum ambayo yale yanawekwa adhabu kama hizo, sasa kwa ujumla lazima adhabu iwekwe wazi ambapo hakimu anayehukumu kesi ile anao uhuru wa kutizama na hiyo ni kuwasaidia wananchi. Kwa sababu unapotaka kutoa adhabu unatizama mambo mengi tu sio lile kosa tu lakini unatizama mambo mengi ya yule mtu ambaye ametenda kosa. Kama ni kosa lake la mwanzo au kama ni kosa ambalo kila siku anafanya au kafanya kwa bahati mbaya, sasa haya yote haya yanakupa wewe kama ni hakimu kutoa ile adhabu kwamba badala ya milioni moja basi sasa angalau uweke laki mbili au laki tatu. Kwa hivyo ukiweka milioni moja tu ni kusema kwamba mtu yoyote yule anayefanya kosa ama kwa bahati mbaya au pengine ni mara yake mwanzo au ni mara yake ya sita zote ziwe hivyo itakuwa kwa kweli si utaratibu mzuri.

Kuna utaratibu ambao unawekwa huo na hakimu anapewa *discretion* ya kufanya mambo hayo kutokana na yule mtendaji na kutokana na kosa wenyewe ambalo amelifanya.

Suala jengine ambalo limezungumzwa ni suala la Mkurugenzi wanasema kutoshtakiwa. Hapa naomba tu Waheshimiwa Wajumbe watizame kwamba hatukusema kwamba Mkurugenzi na wenzake hawatoshtakiwa aa. Tulisema wakati wa utekelezaji wa shughuli zao pale ambapo kwa bahati mbaya unaweza ukawa unatekeleza shughuli zako lakini kwa bahati mbaya ukakosea kitu au ukaongeza kitu, sasa ile haitochukuliwa kwamba umefanya kosa la kimakusudi. Ndio huyu Mkurugenzi na wasaidizi wake wamepata *exemption* hiyo. Lakini sio kwamba unapofanya makosa mengine kwamba ukifanya kosa la rushwa na nini kama hutshtakiwi aa. Ukisoma kifungu cha 19 naomba ukisome vizuri kinaelezea wazi kwa yale mambo ambayo unatakiwa uyafanye kwa bahati mbaya ukasahau imeandikwa hasa hatoshtakiwa kwa kosa la kutenda au kuacha kutenda kwa nia nzuri wakati wa utekelezaji wa shughuli zao. Si kwamba ni *general* hii kwamba kila kitu hutoshtakiwa huisemi hivyo na wala haiwi hivyo.

Mhe. Fatma Mbarouk ninamshukuru kwa michango yake na maoni yake na tutayazingatia hayo. Pia ninamshukuru Mhe. Panya kifungu cha 8(1) alizungumzia sana hasa katika kifungu cha 1(b), hapa ninachotaka kusema kwamba ni kweli Mkurugenzi Mtendaji anayo haki hiyo ya kukataa kusajili lakini tumesema kwamba akikataa kusajili basi lazima atoe sababu, sababu gani. Sio tu kwamba kama mtu anamchukia kama alivyosema akasema sisajili, itabidi lazima utoe sababu na sababu ile akaridhika sawa lakini kama hakuridhika anaweza akakata rufaa kwa Waziri.

Sasa ushauri wao kwa kusema kwamba tufanye bodi ya kupitia na nini hii Mhe. Mjumbe tunahisi si nzuri kwa sababu hapa tuna-*deal* na shughuli za biashara, na biashara hazitaki zicheleweshwe. Ukianza kuweka bodi unaweza ukachelewa sana, bodi mpaka ikutane ikae inaweza ikachukua wiki mbili tatu, kitu kama hicho kwa kweli kitawavunja moyo sana wafanyabiashara. Na ndio maana tumefanya sheria hizi ile iliyopitishwa juzi ya Usajili wa Biashara na hii ili wale wafanyabiashara sasa waje katika shughuli za uandikishaji biashara hapa Zanzibar. Kwa sababu zamani ilikuwa usajili wenyewe unachukua muda, shughuli zenyewe zote zinachukua muda, kwa hivyo wafanyabiashara wengi wa makampuni hayo walikuwa hawaji kusajili hapa Zanzibar. Kwa hivyo tulikuwa tunakosa *fee*, tunakosa mapato. Kwa hivyo hili Mhe. Mjumbe Bi. Panya tukifanya hivyo tutarejea kule kule nyuma lakini tumerahisisha haya ili watu waweze kufanya shughuli zao haraka haraka na kuweza kusajili.

Kwa hivyo mimi ninafikiri kifungu cha 8 (2) kinatoa usuluhisho wa suala lako. Kwa sababu kama inatolewa sababu na Mkurugenzi Mtendaji basi ikiwa hukuridhika una haki ya kukata rufaa kwa Waziri, na Waziri pale pale akaishughulikia na anaweza akatoa maamuzi au maagizo mengine.

Ninamshukuru pia kwa kusema kwamba kanuni ziharakishwe, ninamuahidi kama nilivyoahidi katika sheria iliyopita kwamba suala hili tunalitizama namna gani ya kuharakisha hizi kanuni tumeshaanza kufikiria utaratibu wenyewe, na zikimaliza kanuni hazitochukua muda mrefu *inshaallah* tutazichapisha.

Mhe. Jaku ninamshukuru kwa maoni yake na suala la kwamba kampuni za wazawa zipewe kipaumbele ni kweli lakini lengo la usajili huu ni kwamba lazima masharti yakamilishwe. Kuna masharti ambayo tutayaweka katika kanuni kama wewe ni mzawa, kama wewe si mzawa ikiwa hujakamilisha masharti yale kwa hivyo hutopata *reference* yoyote ile. Na hiyo ndio itatusaidia sisi kama ni serikali kuweza ku-*monitor* zile kampuni kwa utaratibu

ule ambao tumesema kwamba kutakuwa na fomu maalum za kujaza. Kwa hivyo Mhe. Jaku tutafanya kwa misingi hiyo.

Na mwisho Mhe. Spika, ninamshukuru Mhe. Hamza kwa mashauri yake hasa alipozungumzia suala la kifungu cha 7 ambacho kifungu cha 7 ni kazi za Mkurugenzi Mtendaji na kazi za Idara kwa ujumla. Lakini kama nilivyosema kifungu cha 7 tukisoma kifungu cha 7(b) (d) na (g) kitatupa muelekeo wote ule ambao ameusema Mhe. Hamza. Kuweka kumbumbu za usajili, madaftari, takwimu, kukusanya na kuwajibika kwa mapato yote kwa mujibu wa sheria na kutathmini kila wakati utendaji na matokeo mazuri ya sheria hizi, haya ndio madhumuni makubwa. Lakini ushauri wake ule wa Wizara ya Biashara mimi ninafikiri ni mzuri, ni suala zuri, mimi binafsi ninalikubali na nitazungumza na Mhe. Waziri wa Biashara na yeye bahati nzuri yupo tutatizama yale mambo ambayo umeyaelekeza namna gani tuweze kuya-*accommodate*, na kama kuna haja basi tutakuita ili tupate mawazo zaidi ni suala zuri ambalo nakubaliana nalo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ninawashukuru tena Wajumbe kwa michango yao mizuri yenye lengo la kuboresha sheria hii na yote tutaichukua na kuifanyia kazi na naomba kutoa hoja na kuwaomba Wawakilishi kwamba waikubali sheria hiyo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar ya Mwaka 2012

Sehemu ya Kwanza
Masharti ya Awali

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili
Uanzishwaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar

Kifungu 3 Uanzishwaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar
Kifungu 4 Kazi za Wakala
Kifungu 5 Matawi ya Ofisi

Sehemu ya Tatu
Uongozi wa Wakala

Kifungu 6 Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7 Kazi za Mkurugenzi Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8 Uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwanza napenda nichukue fursa hii kumshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pamoja na hayo nilikuwa mimi bado ninamshauri kwa kuepusha nilisema Mkurugenzi Mtendaji ni binaadamu kama binaadamu mwengine yeyote, kama ile bodi itakuwa ni kitu kikubwa japo kuunda kamati ambayo itaweza kumrahisishia yeye katika majukumu yake ya kupitisha majina yale ya usajili, kwa

kuepusha hata rushwa kama atakuwa yeye yuko peke yake nahisi yanaweza yakajengeka mambo ya upendeleo, rushwa. Kwa hivyo nilikuwa bado Mhe. Waziri ninakushauri juu ya hilo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Panya ni mazuri lakini katika suala la utendaji huwezi utendaji ukauanza kwa bodi. Sasa mimi nahisi kwa sababu huyu ni mtendaji aachiwe zile shughuli zake zote azifanye kiutendaji pale ambapo pana matatizo kama utaratibu wa utendaji ulipo unakata rufaa kwa mkubwa wake, na ndio maana tukasema akitoka Mkurugenzi Mtendaji kama ametoa uamuzi, kitu tulichomtaka kwamba lazima atoe maelezo kwa maandishi kwa nini akakataa. Maelezo yale yatakufanya wewe uridhike ama usiridhike, hukuridhika unakata rufaa kwa Waziri, na hata kwa Waziri kwa mujibu wa katiba yetu si *final* kama hukuridhika unayo ruhusa ya kwenda kwengine. Sasa yale maamuzi yale ambayo yatatolewa ndio muhimu ambayo yanatakiwa. Sasa mimi ninafikiri tuache hii katika mtiririko wa utendaji kuliko kufanya bodi ambayo bodi itachukua muda na ambayo itakuwa katika mtiririko tofauti kabisa na utaratibu wa kiutendaji.

Mhe. Panya Ali Abddalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti bado ninaendelea kumshukuru Waziri kwa majibu yake, lakini Mhe. Waziri alipokuwa anajibu hizi hoja alisema alichokuwa anahofia kwanza ni kujali muda ambao imeundwa hii ili iweze kuharakisha muda, lakini hapa alinambia majibu yapo katika kifungu namba 2 ambayo mtu ataruhusiwa kutoa malalamiko kama atakuwa hakuridhika na yale majibu ya Mkurugenzi Mtendaji. Lakini naona itazidi kuchukua huo muda kwa sababu hizo siku 21 za kuweza kukaa yeye ili akaripoti kwanza kwa Waziri pengine hakuridhika zaidi aende tena mahkamani sio muda unazidi vile vile.
Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba arejee sijalifahamu.

Mhe. Spika: Mhe. Panya hebu tupe maelezo yako vizuri ili Waziri apate kufafanua.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu nilikuwa nikisema aunde bodi lakini kwa kuwa yeye kasema bodi inaweza ikachukua muda mrefu, nikasema japo kuweza kuunda kamati ndogo ambayo itaweza kumrahisishia yeye huyu Mkurugenzi Mtendaji ili aweze kufanya kazi zake kiuhalali na asipate hoja nyengine zozote kwa sababu ile kazi haikufanya peke yake amesaidiwa na wenzake. Lakini Mhe. Waziri akasema kwanza kuunda bodi kutafanya kucheleweshe, itabidi bodi mpaka ikutane sijui na nini, nikasema sawa lakini na hii pia ambayo inasababisha pia itaharakisha muda inabidi huyo mlalamikaji kama hakurudhika na majibu ya Katibu Mtendaji ina maana akae siku ishirini na moja kwanza aweze kupeleka malalamiko yake. Lakini pia kama ikiwa hatoridhika tena aweze kwenda ngazi ya juu zaidi si itakuwa ndio ile ile inapoteza muda.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti naomba nikisome kifungu cha pili ambacho kinasema mtu yoyote asiyeridhika na maamuzi ya Mkurugenzi Mtendaji anaweza kuwasilisha madai yake kwa Waziri ndani ya siku 21. Yaani kama leo umepewa yale majibu hukuridhika leo leo unaweza kwenda kwa Waziri lakini isizidi siku 21 ndio madhumuni yake kwa hivyo hii haicheleweshi. Ukipewa jibu leo, leo unaweza ukaenda kwa waziri, kesho unaweza ukaenda kwa Waziri mpaka zikifika siku 21 kama hujenda ndio huwezi tena kwenda ndio madhumuni ya kifungu hiki. Kwa hivyo hii ni kuthibitisha zaidi kwamba tunafanya haraka haraka. Ninakushukuru.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 8	Uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji
Kifungu 9	Kutoa Mamlaka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10	Uteuzi wa Naibu Mkurugenzi Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11	Uteuzi wa Naibu Mrajis Dhamana Pemba
Kifungu 12	Wasaidizi Mrajis
Kifungu 13	Uteuzi wa Maafisa wengine

Sehemu ya Nne
Masharti ya Fedha

Kifungu 14	Fedha za Wakala
Kifungu 15	Mapato yanayolipwa katika Mfuko Mkuu
Kifungu 16	Makadirio
Kifungu 17	Hesabu na Ukaguzi

Kifungu cha Tano
Masharti Mengineyo

Kifungu 18	Taratibu za Usajili na Madaftari ya Usajili
Kifungu 19	Kinga kwa Makosa
Kifungu 20	Uhalali wa Nyaraka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21	Ukabidhi wa Raslimali na Madeni
Kifungu 22	Mashauri yanayosubiri
Kifungu 23	Makosa na Adhabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 24	Kanuni
Kifungu 25	Marekebisho yatokanayo
Kifungu 26	Akiba

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imepitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara
na Mali Zanzibar kwa Mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar wa 2012 usomwe mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nikupongezeni nyote kwa kazi nzuri ya kumaliza mswada huu kwa kipindi kilichoishia saa hizi karibu saa sita na nusu. Kwa hivyo kwa leo Katibu anatwambia hakuna shughuli nyengine, lakini kabla ya kuakhirisha shughuli yetu basi nitoe taarifa fupi kwamba Waheshimiwa Wajumbe Wanawake tunaombwa na Katibu wa UWAWAZA tubaki kidogo humu ndani kuna taarifa muhimu Katibu atakuja kuitoa mara baada ya kuakhirisha shughuli yetu hii.

Waheshimiwa Wajumbe basi baada ya shughuli hii naomba sasa tusitishe shughuli zetu hadi tarehe 16/10/2012 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 6.32 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 16/10/2012 saa 3.00 asubuhi)